# TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA TAMTHILIA ZA *NGUZO MAMA* NA *MAMA EE*.

**NA**

**CHACHA WILSON CALEB.**

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHOLEZA BAADHI YA MAHITAJI YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

NOVEMBA 2013

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo chochote kile, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Chacha Wilson Caleb. Tarehe.

________________________ ________________________

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Dkt.Evans M. Mbuthia Tarehe.

________________________ ________________________

Dkt. Francis Mwangangi Musyoka Tarehe.

________________________ ________________________

# KUTABARUKU.

Nawatabarukia wazazi wangu wote wanne; marehemu babangu Caleb Samburu Roswe,

Mama mzazi Esther Gati Caleb, baba mkwe Pastor Charles Marwa na marehemu mama mkwe Selina Sibora Marwa.

Tabaruku nyingine ni kwa mke wangu Mary Chacha na watoto wetu David, Dorcas, Catherine, Selly, Esther na Caleb Samburu. Mke wangu na wazazi wamenitunza na kuniunga mkono kwa hali na mali wakati wa kipindi kigumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu. Nawatakia heri na Baraka za Mwenyezi Mungu wale wote walio hai.

# SHUKRANI.

Namshukuru  mwenyezi Mungu kwa kutupatia karama yake ya uhai, hekima na busara. Bila haya yote hatungeweza kufikia kiwango ambacho tumefika. Kwa hivyo hatuna budi kumshukuru.

Ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Mbuthia Evans M. na Dkt. Mwangangi Musyoka kwa kujitolea kwao kuniongoza na kunipatia mwelekeo uliozalisha mafanikio ya kazi hii. Haingekuwa kazi rahisi kuandika tasnifu hii bila ushauri na uongozi wao. Tena nawashukuru walimu wangu wote walionifundisha tangu nijiunge na masomo ya uzamili mwaka 2011. Walimu hawa ni Dkt Iribemwangi, Dkt Jefwa Mweri, Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Amir Swaleh, Prof. Kineene wa Mtiso na Prof. John Habwe miongoni mwa wengine

Mafunzo ya Dkt. Zaja yalinifaa sana wakati wa kuandika tasnifu hii kwa sababu kuna upungufu wa matini zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, hasa zile zinazohusiana na nadharia mbalimbali.

Matini nyingi zinazohusiana na nyanja ya nadharia zimeandikwa katika lugha ya kingereza. Kwa hivyo ilinibidi nizisome na kutafsiri kutoka kingereza hadi Kiswahili jambo ambalo halikuwa rahisi. Ndio maana nasema kuwa ujuzi alionipa Dkt. Zaja ulinifaa sana kwa kazi hii na zingine pia. Siwezi nikaisahau familia ya shemeji, wakili Enock Chacha kwa kunitunza muda huo wote niliokuwa nikiendelea na masomo yangu. Shemeji Miriam Mwita-V.C. chuo kikuu cha Afrika Mashariki Baraton alinitia shime ya kuendelea na masomo kuanzia shahada ya kwanza hadi shahada hii ya uzamili. Mungu ampe baraka kulingana na mapenzi yake.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioshirikiana hasa baada ya kunitambua na kunichagua kuwa kiongozi wao. Changamoto nilizokumbana nazo ni nyingi lakini haya yote niliyaweza kwa sababu ya Mola wetu anitiaye nguvu na kunipa uwezo. Orodha ni kubwa lakini natamatisha kwa kuwashukuru Amos G. Mariba-deputy P.C. Nairobi, Nelson Marwa-Regional Commissioner Coast, Mangiteni Joseph-KNUT Executive secretary-Kuria Mashariki. Sina lugha ya kujieleza jinsi ninavyohisi kuhusu msaada wenu ila nawaombea dua njema kwa Mola wetu.

# IKISIRI

Tumeangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee. Jamii mbalimbali zina mtazamo anuai kuhusu taswira ya mwanamke. Waandishi wa tamthilia hizi walitoka maeneo tofauti na waliandika katika vipindi tofauti, lakini kazi zao zinashabihiana sana.

Tulichagua mada yetu ili kuchambua na kuchanganua tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee kwa sababu ya fani na maudhui yanayoashiria jinsi hali halisi ilivyo katika jamii zetu. Malengo ambayo tumeyaangazia ni jinsi changamoto mbalimbali zinamkabili mwanamke na kumzuia kupata haki, jinsi asasi za kijamii zinavyochangia mwanamke kutopata mafanikio katika harakati zake za kutaka kujikomboa na kuonyesha jinsi baadhi ya waandishi wamemsawiri mwanamke kwa njia mbalimbali kama vile shujaa, mwongo mwoga na kadhalika.

Tuliweza kujikita kwenye vitabu hivi viwili tu, *Nguzo Mama* na *Mama Ee* isipokuwa pale tulipohitaji kutoa idhibati au mifano zaidi. Dira iliyotuongoza kuangazia mada yetu ni nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliyoasisiwa na Georg Lucaks mwanaitifaki wa Karl Marx. Nadharia hii ya Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalum cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina sya kazi ya sanaa hasa fasihi, umma na muundo wa kijamii.

Baadhi ya changamoto tulizofanikiwa kugundua katika uchambuzi wetu ni matatizo ya unyumba, ubaguzi wa kijana wa jinsia ya kike, mila na desturi katika ndoa, dini katika mahusiano ya kinyumba, mahakama za kiserikali na zile za kijijini, ukosefu wa umoja na ushirikiano, utabaka,na majukumu mengi miongoni mwa zingine. Asasi za kijamii hasa ndoa na tamaduni zilionekana kuchukua nafasi ya vizingiti vikuu na kumfanya mwanamke kuwa na taswira mbalimbali. Kwa mfano mwanamke amechorwa kama mwoga, mwenye chuki na wivu, mwenye tamaa, mwenye mashaka na mdhaifu miongoni mwa nyingine.

Tulitamatisha kazi yetu kwa kutoa mapendekezo mawili. Pendekezo la kwanza linahusiana na dini. Swala la dini kuchangia katika unyanyaswaji wa mwanamke yafaa lichunguzwe kwa undani zaidi. Pendekezo la pili linahusiana na suluhu la kudumu kuhusu changamoto zinazomkumba mwanamke katika jamii na kumnyima uhuru kamili.

# YALIYOMO


MADA ….…………………………………………………………………. (i)

UNGAMO……..…………………………………………………………….. (ii)

KUTABARUKU…………………………………………………………. (iii)

SHUKRANI……………………………………………………….………. (iv)

IKISIRI……………………………………………………… …………… (v)


## SURA YA KWANZA


1.1 UTANGULIZI…………………………………………………….……. 1

1.2 TATIZO LA UTAFITI…………………………………………………… 2

1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI…………………………………………… 3

1.4 MASWALI YA UTAFITI………………………………………………… 4

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII ………………………………… 4

1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI WETU …………………………… 5

1.7 MSINGI WA NADHARIA ………………………………………………. 5

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII ………………………………. 10

1.9 MBINU ZA UTAFITI ……………………………………………….... 17

1.10 HITIMISHO …………………………………………………………... 17


## SURA YA PILI


UCHAMBUZI WA TAMTHILIA YA MAMA EE ……………………………… 19

2.0 UTANGULIZI…………………………………………………………... 19

2.1 MATATIZO YA UNYUMBA ………………………………………….....20

2.2 UBAGUZI WA KIJANA WA JINSIA YA KIKE ……………………….. 27

2.3 NAFASI YA MILA NA DESTURI KATIKA NDOA …………………... 29

2.4 NAFASI YA DINI KATIKA MAHUSIANO YA KINYUMBA ………... 33

2.5 NAFASI YA MAHAKAMA KATIKA SWALA LA NDOA NA UNYUMBA ……………………………………………………………36

2.6 UMOJA WA WANAWAKE …………………………………………….. 39

2.7 KIMALIZIO ……………………………………………………………..41

## SURA YA TATU

UCHAMBUZI WA TAMTHILIA YA NGUZO MAMA 47

3.0 UTANGULIZI …………………………………………………………………47

3.1 SWALA LA UTABAKA NA WANAWAKE …………………………...........48

3.2 TAASHIRA YA UMOJA ………………………………………………………..52

3.3 WANAWAKE NA WATOTO WA KAMBO ……………………………...57

3.4 MAJUKUMU YA MWANAMKE NA NAFASI YAKE KATIKA JAMII …………………………………………………………….62

3.5 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NGUZO MAMA …………….. 65

## SURA YA NNE

WAHUSIKA NA MANDHARI KATIKA TAMTHILIA ZA NGUZO MAMA NA MAMA EE ……………………………………………….. 69

4.0 UTANGULIZI ……………………………………….………………..69

4.1 DHANA YA WAHUSIKA …………………………………………………...69

4.2 MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA MAMA EE NA NGUZO MAMA ………………………………………………………….70

## SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 UTANGULIZI ……………………………………………….………….75

5.1 MUHTASARI WA KAZI HII …………………………………….………….75

5.2 HITIMISHO ………………………………..…………………............76

5.3 MAPENDEKEZO ………………………..…………………….............77

MAREJELEO …………………………………………………………..78

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Mada tunayochunguza inahusu taswira ya mwanamke katika tamthilia mbili teule; *Nguzo Mama* ya Penina Muhando (1982) na *Mama Ee* ya Ari Katini Mwachofi (1987). Jamii tofauti zina mtazamo anuwai kuhusu taswira ya mwanamke. Kwa mujibu wa Msokile, M. (1993) 'taswira' ni neno lenye matumizi mbalimbali katika uhakiki wa fasihi. Kulingana na Kimani Njogu na Rocha Chimera (1993), 'taswira' ni mkusanyiko wa picha zinazotokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Vile vile, taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji wa kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi huwa na funzo au ujumbe fulani.

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili sanifu (2002), taswira ni picha ya mambo au vitu vinavyomjia mtu akilini mwake; maono, picha. Pia ni mchoro, sanamu.
Maana ya kijumla ya neno hili taswira ni: mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake ya fasihi.

Tutajikita kwenye tamthilia hizi na kuzitumia kama kielelezo hata ingawa tutarejelea matini zingine ambazo zina maudhui yanayokaribiana kwa sababu mambo ya kimsingi ya kibinadamu ni yale yale tu, ila mazingira ndiyo hutofautiana.  Changamoto zinazowakabili wanawake zinaweza kutofautiana kimaeneo lakini ukweli ni kwamba zipo ulimwenguni kote. Jamii tofauti zimeweka mikakati ya kutatua matatizo yanayowakabili wanawake lakini hata hivyo utamaduni ni kizingiti kikubwa katika swala hili; hasa katika ulimwengu wa tatu. Juhudi nyingi zimefanywa na wanaharakati wasomi pamoja na wanajamii hususan baadhi ya wafuasi wa dini mbalimbali ili

kuboresha nafasi ya mwanamke katika jamii lakini juhudi hizo hazijafaulu kwa kiasi kikubwa. Kuna mambo ya ukale na usasa ambayo yamesababisha baadhi ya matabaka kudai haki zao. Madai haya yameleta athari katika jamii na tutachunguza kama ni hasi au chanya kwa kuegemea kigezo cha kifamilia hasa kutoka kwa matini teule.

Fasihi inaweza kutumika kama dira ya kutuongoza kuchunguza jamii au wahusika fulani. Tutatumia tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee* kumulika changamoto, uozo au maovu yanayowakumba wanajamii wetu hasa wa jinsia ya kike. Kwa muktadha huu, sisi tutaangazia 'taswira ya mwanamke' katika tamthilia ya *Nguzo Mama* na *Mama Ee.* Tutaangazia jinsi mwanamke anavyomithilishwa kwa kuchunguza matendo anayotendewa.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Migogoro inayopatikana katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee* inashabihiana kwa kiwango kikubwa licha ya kuwa waandishi wake wanatoka maeneo tofauti na waliandika katika vipindi tofauti. Kazi hizi zimetupatia msukumo wa kutaka kufanya uchunguzi kwa kusudi la kupata uelewa zaidi kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wanawake katika jamii nyingi zenye tamaduni tofauti nchini mwetu. Sisi tumeamua kuyaita matatizo yanayowakabili wanawake; "changamoto". Hii ni kwa sababu hayaishi licha ya kwamba yamekuwa yakishughulikiwa na wanaharakati hasa wa mirengo ya kifeministi kwa kipindi kirefu kinachokaribia miongo mitano iliyopita kuanzia mwaka 1975 hasa katika Ulimwengu wa Tatu. Suluhu la kudumu halijapatikana licha ya juhudi hizi.

Katika utafiti ambao tumeufanya, tumegundua kuwa waandishi wengi wameandika juu ya harakati za wanawake kujikomboa kutokana na matatizo yanayowakabili, jinsi mwanamke amesawiriwa na waandishi mbalimbali na mikakati wanayotumia wanawake kujikomboa. Wametumia nadharia ya ufeministi na ile ya umuundo lakini uchunguzi wa maswala yanayowakumba wanawake haujafanywa kwa wingi kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Tunaamini kuwa nadharia hii itatusaidia katika uchambuzi wetu wa jinsi migogoro mingi imejitokeza katika tamthilia tulizotaja.

Migogoro inayopatikana kwenye tamthilia hizo ni kielelezo cha yale yanayopatikana katika jamii za waandishi. Maswala haya yanaendelea kuangaziwa na waandishi na wahakiki. Maswala ya wanawake yamekuwa yakiangaziwa sana kwa miaka ya hivi karibuni hadi sasa. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanajamii hawajakuwa na mwamko wa kutosha kuwasaidia kutambua haki zao kikamilifu na kuzitetea. Kile kinachosababisha ukosefu huu ni mazoea mabaya pamoja na kifungo cha mila na desturi.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Tunadhamiria kuchambua na kuchanganua tamthilia mbili *Nguzo Mama* na *Mama Ee* kwa kuangazia taswira ya mwanamke ili:-

i. Kubainisha jinsi changamoto zinazowakabili wanawake zimechangia kutofaulu kupata haki zao.

ii. Kubainisha kuwa majukumu anayopewa mwanamke kupitia asasi za kijamii yanachangia sana mwanamke kutopata mafanikio katika harakati zake.

iii. Kuonyesha jinsi baadhi ya waandishi wamewasawiri wanawake kama mashujaa.

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

(i) Ni sababu zipi zimechangia kutopatikana suluhu mwafaka juu ya changamoto zinazowakabili wanawake?

(ii) Ni jinsi gani watunzi wamewasawiri wanawake katika kazi zao ili kuonekana mashujaa katika harakati za kupigania haki zao?

(iii)Ni majukumu yapi ambayo wanawake wamepewa kupitia kwa asasi za kijamii yanayochangia kutopatikana mafanikio kwenye harakati zao?.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tumechagua mada hii ili tuchambue na kuchanganua tamthilia tulizoteua kwa sababu ya fani na maudhui yake ambayo yanaashiria jinsi hali halisi ilivyo katika jamii zetu. Katika baadhi ya kazi za kifasihi, aghalabu mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu, mnyonge, mtu asiye na haki, mwoga na pia kama chombo kisichothaminika. Wakati mwingine wasanii huwachora wanawake kama watu wanaodharauliana na kukosa ushirikiano baina yao. Masuala haya yametupatia msukumo wa kuangazia kinachosababisha mitazamo hii miongoni mwa baadhi ya waandishi. Si vyema kuona wanawake wakipitia maisha magumu yanayosababishwa na binadamu mwenzake na kupuuzilia ; mwanamke ni nguzo muhimu ya jamii na taifa lolote lile. Ni vizuri atunzwe na kusaidiwa ili kuwa na jamii yenye mshikamano. Kulingana na Hough, G. (1962:6),

> *"Hakuna kazi yoyote ya uhakiki wa fasihi iliyokamilika. Uhakiki haushughulikiwi wakati mmoja na kuisha kabisa kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia. Fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya…."*

Kauli hii inatupatia nguvu za kufanya utafiti kuhusu mada ya taswira ya mwanamke kwa kutumia vielelezo vyetu na kumulika jamii na jinsi mwonoulimwengu wake ulivyo kuhusu mwanamke.

Kuna madai kwamba wandishi wengi wa jinsia ya kiume hasa tukiwarejelea waasisi wa kazi za tamthilia kama vile Aristotle, waliweka misingi ya uandishi wa tamthilia. Waliainisha tamthilia katika makundi mawili; tamthilia za kitanzia na tamthilia za futuhi.Tamthilia zilizofungamana na futuhi zilikuwa za vichekesho na ziliwahusu wanawake na watoto. Kuanzia kipindi hicho, hali ya kuwadhalilisha wanawake ilishika kasi kupitia kazi zilizoandikwa ili kutimiza malengo haya ya vichekesho. Mtazamo na mwamko mpya ulileta na wanaharakati wa utetezi wa haki za wanawake. Ndiposa tunawapata waandishi kama Reed E. (1970) akiandika "*Problems of Women's Liberation*", Millet K. (1971) akiandika "*Sexual Politics*" na Toril (1985) akiandika "*Sexual/Textual Politics*" miongoni mwa nyingine.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI WETU

Katika utafiti huu tutajishughulisha na vitabu hivi viwili- *Nguzo Mama* na *Mama Ee*. Pia tutajishughulisha na vitabu ambavyo vimeandikwa na wandishi wengine ikibidi ili kutoa ithibati au mifano ya ziada. Tutajishughulisha na baadhi ya vipengele vya fani hususani wahusika, mandhari na maudhui kwa ujumla.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Tutaishughulikia kazi hii tukiongozwa na nadharia ya 'Sosholojia ya Fasihi'iliyoasisiwa na Georg Lukacs. Lukacs alirithi mawazo ya maendeleo ya kijamii na migongano ya kitabaka

kutoka kwa Karl Marx. Kwa mujibu wa Coser L. (1963) Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalumu cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina ya kazi ya sanaa, umma na muundo wa kijamii na jinsi kazi hiyo imejitokeza na kutathminiwa ubora na uhafifu wake. Hunuia kueleza sababu ambazo zimechangia kuibuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo la kijamii na jinsi fikra za ubunifu wa mwandishi huongozwa na mila, desturi na mpangilio wa jamii husika. (Hii ni tafsiri yetu).

Kulingana na Coser (1963), binadamu ndiye kiumbe pekee aliye na uwezo wa kutumia lugha. Kwa miaka mingi iliyopita, binadamu amekuwa akijishughulisha na ukusanyaji wa maarifa pamoja na kanuni za mwenendo maishani. Haya yote yameweza kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Anatamatisha kauli hii kwa kusema kwamba ni jamii za kibinadamu pekee zilizo na uwezo wa kuwa na mila. Tylor E. kama alivyonukuliwa na Coser (1963) kuhusu Sosholojia ya Fashi alitoa mchango kuhusu dhana ya utamaduni kwamba, ni dhana isiyoweza kuelezwa kwa urahisi kwa sababu ni changamano. Inahusu imani, mila, desturi, itikadi, maadili, sheria, elimu pamoja na mazoea ambayo mtu huwa nayo kama mmoja wa wanajamii. Vipengele hivi ni muhimu kwetu kwa sababu vitatusaidia kuangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee*. Jamii zote zinazojulikana zimewaweka wanajamii katika matabaka kihadhi. Kuna tabaka la juu, kati na chini. Mchakato huu unahusu ugavi wa majukumu ya kila mtu kiumri, kijinsia na kihadhi huku utofauti ukibainika wazi kupitia umiliki wa mali, mamlaka na ukuu. Tofauti kati ya tabaka la juu na la chini, matajiri na maskini, watawala na watawaliwa, wenye nguvu na wanyonge ni vigezo vinavyotumiwa kuainisha makundi haya. Jinsi wanajamii katika makundi haya wanavyochukuliwa na kuhudumiwa, wanavyogawiwa majukumu na ukosefu wa haki sawa hubainisha mfumo wa kijamii.

Sosholojia ya Fasihi pia huangazia mamlaka na nguvu kama mihimili ya kijamii. Kwa mujibu wa Coser (1963), mamlaka ni uwezo wa kuamua mwenendo au tabia ya watu wengine kulingana na matarajio ya mwenye mamlaka. Hakuna mahusiano ya kijamii ambapo elementi ya mamlaka itakosekana kabisa; hivyo basi kuna fikra kwamba dhana ya mamlaka ni msingi katika dhana zote za kisosholojia. Kwa kifupi,mamlaka ni zile nguvu ambazo mtu hupewa kulingana na kaida zinazokubalika na watu wawili au zaidi na kati ya makundi mawili au zaidi kwenye mahusiano. Coser (1963) anamnukuu Max Weber aliyeainisha mamlaka na kuyaweka katika makundi matatu ambayo ni mamlaka ya kisheria, mamlaka ya mila na desturi (mapokeo) na mamlaka ya kihaiba (charismatic).

Narizvi (1982) aliandika kuwa: uhusiano baina ya fasihi na jamii umekuwa mada ya mvuto katika uchunguzi wote wa kibinadamu.Wahakiki wa kazi zilizoandikwa na wanasosholojia wamekuwa wakijadili mada hii kutokana na mitazamo mbalimbali na kutoa kauli mbalimbali zenye kweli kinzani kiasi cha kumkanganya mtu aliye na tajriba katika nyanja mahususi.

Kulingana na Wellek na Warren (1954), uhusiano baina ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kutanguliza ufungamano wa fasihi na jamii. Wahakiki wa dhana hii wanadai kuwa ni makosa kuchukua fasihi kama kigezo cha kuashiria jinsi jamii yoyote ile ilivyo. Walidai kuwa kazi kama zile za mwandishi maarufu Shakespeare na tenzi za Milton au kazi ya Burke haziwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha jamii zao. Jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea tajriba, uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha hivyo basi itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka.

Mtazamo wa fasihi kupitia sosholojia, hutufanya tumchukue mwandishi kama zao la nguvu za kisosholojia za wakati wake na kuepuka kumpunguzia sifa za ubunifu asilia.

Kulingana na James Sutherland (1957), “jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopokea pamoja na dini yake”.
Pingamizi nyingine kuhusu matumizi ya elimujamii ya fasihi ni mtazamo wa mwandishi na nguvu za kisosholojia ambazo huchunguza sehemu teule na hivyo kuufanya mtazamo wa kijumla kukosa maana. Wahakiki wanashikilia dhana kwamba uchunguzi wa fasihi unahitaji tuwe na wazo kuhusu kile ambacho ni muhimu na kile ambacho si muhimu. Wahakiki wanaopinga mbinu ya kisosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi upande mmoja na hali ya kijamii, uchumi na siasa upande mwingine.

Uchunguzi wa kijamii kuhusu kazi ya maandishi au mwandishi mwenyewe utatusaidia kumchunguza mwandishi kama mwanachama wa jamii, athari za kijamii zilizomwathiri na kumpatia msukumo wa kubuni kazi ya sanaa. Kwa mfano sisi tutachunguza kazi za Muhando na Mwachofi ambazo ni za kisanaa. Sosholojia ya Fasihi inamzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa ulimwengu huu na sanaa kwa ujumla wake. Ndio maana tumeichagua nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kutupatia msingi kuzichambua na kuzichanganua tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee*, kwa kuegemea mihimili yake.

Kulingana na Mbuthia (2005), juhudi kubwa zimefanywa ili kupata uelewa zaidi kuzihusu jamii kupitia uchunguzi wa kina wa kazi ambazo zimeaandikwa, hii inawezekana tu ikiwa mtafiti atachagua nadharia inayofaa. Kazi za Wellek na Warren (1963) zinabainisha uwezo wa

Sosholojia ya Fasihi kuchanganua maswala haya. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi itatufaa kwa kazi hii tunayoishughulikia. Kwa mujibu wa Wellek na Warren (1963:94);

> *Fasihi imeibuka kutokana na uhusiano wa karibu wa taasisi za kijamii na jamii duni. Ni vigumu kutofautisha ushairi na ibada, mazingaombwe na kazi au igizo. Fasihi pia ina dhima katika jamii na haiwezi kuwa ya mtu binafsi, hivyo basi, maswala mengi ambayo huibuka kupitia uchunguzi wa kifasihi huwa ya kijamii. Kwa mfano maswala kuhusu mila, kaida, hadithi, msimbo na visasili. (Tafsiri yetu)*

Kama nadharia yoyote ile, Sosholojia ya Fasihi ina wale wanaoipinga. Wapinzani wake wanadai kwamba, nadharia hii haitusaidii kuchunguza uhusiano baina ya fasihi na mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa sababu uhusiano hauwezi kujitokeza wazi katika kitengo chochote kile na hivyo basi umuhimu wake hauwezi kutathminiwa. Kwa mfano, katika kazi fulani, mada hujikita kwenye maswala ya kisiasa, kijamii, au mahusiano ya kiuchumi. Huu ni ukweli ingawa Sosholojia ya Fasihi haiwezi kugusia suala la umuundo au maumbo.

Tungependa kutamatisha sehemu hii kwa kusema kwamba maelezo ambayo tumetoa hapa kumhusu Georg Lukacs yanatokana na athari ya itikadi za ki-Marx. Mawazo ya wanafalsafa kama vile Pierre Macherey, Terry Eagleton na Fredrik Jameson pia yalitoka kwa Marx na yakaelekezwa kwa fasihi ya wakati huo. Mawazo ya Lukacs ya kuchapisha maandishi kuhusu *'Nadharia ya fasihi'* (1916) yalileta mwamko uliosababisha kuanzishwa kwa shule ya Frankfurt mnamo mwaka wa (1923) na wanasosholojia wa vitengo vyote vinavyohusiana na sosholojia.

## 1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kulingana na Woolf kama alivyonukuliwa na Coser (1963), "mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Kwa ujumla katika jamii nyingi ulimwenguni, nyenzo zote za kuzalisha mali zinatawaliwa na wanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Hali hii huwakumba wanawake kwa sababu tangu zamani wanawake wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi". Woolf kama alivyonukuliwa na Coser anapendekeza kuwa; mwanamke apewe uhuru wa kiuchumi ili aepuke unyanyaswaji na dhuluma. Iwapo jamii itakubaliana na wazo hili la Woolf, ni bayana kuwa unyanyasaji na dhuluma kwa mwanamke utapunguzwa kwa kiwango fulani. Vile vile jamii nyingi za kisasa zimehamasishwa na zimeaanza kuwa na mtazamo chanya wa kuwapatia wanawake fursa ya kujiendeleza kiuchumi kupitia uundaji wa vikundi vya wanawake kama itakavyobainika kwenye uchunguzi wetu.

Kwa mujibu wa Beauvoir (1949), utiifu hauhusishwi miongoni mwa majukumu ya mwanamke. Alidai kuwa, kila mwanamke nchini Ufaransa ana uhuru wa kujiamulia mambo lakini nyanjani uhuru huo haupo. Ni uhuru kidhahania kwa sababu hauambatani na uhuru wa kiuchumi. Mwanamke anayemtegemea mumewe hawezi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo kwa sababu mila na desturi hazimruhusu. Hali kama hii ni yakini katika baadhi ya mataifa na jamii hususan bara la Afrika. Uhuru ambao ni hasi haujaleta mabadiliko kwa mwanamke. Amekubaliana na hali yake ya kuwa mwanamke huku akiishi kwa kuvumilia matatizo mengi. Ni kupitia kwa ajira ambapo mwanamke ataweza kujinasua kutokana hali na ya unyanyasaji unaotokana na mila. Hakuna njia nyingine mwafaka ambayo inaweza kumhakikishia uhuru wake maishani isipokuwa hiyo ya ajira. Pindi tu atakapoacha kuwa mtegemezi na kujitosheleza katika baadhi ya mahitaji,

mfumo wa kutegemewa utabadilika na hatakumbana na madhila mengi yanayohitaji kuangaziwa au mtu wa kutegemea kuleta suluhu la masaibu yanayomkumba duniani. Kule kumtegemea mwanamume ndiko huyu mwanaharakati anadai kuwa ni chanzo cha unyonyaji. Jamii haijaweka mikakati ya kutosha ili kuleta mabadiliko kuhusu hali ya wanawake kutumishwa.

Kazi hii ya Beauvoir ni muhimu kwetu kwa sababu ametaja unyanyasaji unaotokana na mfumo wa kijamii. Unyanyasaji ni kipengele miongoni mwa vipengele tulivyovichunguza kama changamoto zinazosababishwa na baadhi ya wanajamii hususani wanaume. Bado ulimwengu huu una baadhi ya sehemu ambazo zinathibitiwa na mifumo ya kijamii ambayo huwakweza wanaume na kuwatweza wanawake. Ni wanawake wachache tu ambao wana imani inayofungamana na misingi ya kisiasa ambao wamechukua hatua ya kujiunga na kuunda vyama vinavyowasaidia kutetea haki zao kama uchunguzi wetu utakavyodhihirisha katika kazi yetu. Haya yote yanaleta mvuto wa kufanya uchunguzi kuhusu hali ya wanawake hasa kuhusu taswira yao kulingana na waandishi mbalimbali. Kazi hii pia ni muhimu kwetu maana itatusaidia kulinganisha na kuchambua taswira ya mwanamke katika *Nguzo Mama* na *Mama Ee*.

Mukobwa (1985) ameshughulikia '*Maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia za Ebrahim Hussein'*. Amezungumzia kipengele cha maudhui ambacho vile vile nasi tutashughulikia huku tukiangazia taswira ya mwanamke. Alitumia nadharia ya ki-Marx kujikita katika uhalisi wa kihistoria, sisi tutatumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ili kutuongoza kuangazia taswira ya mwanamke. Tunakubaliana na ufafanuzi wake kuhusu taswira ila yeye amekusanya data ya utafiti wake kutoka tamthilia za Hussein, mwandishi wa jinsia ya kiume na sisi tutakusanya data ya utafiti wetu kutoka tamthilia moja ya Penina Muhando na nyingine ya Ari Katina Mwachofi

wote wakiwa waandishi wa jinsia ya kike. Kipengele cha maudhui kitatusaidia kuyachunguza mawazo ya Muhando na Mwachofi kutokana na usawiri wao wa mwanamke.

Chesaina (1987) alitumia tamthilia ya Mlama (1972) *'Hatia'* na tamthilia ya Muhando (1982) '*Nguzo mama'* na kueleza utata unaomkabili mwanamke katika hali zake zote za maisha. Tofauti na yeye ni kwamba sisi tutatumia *Nguzo mama* na *Mama Ee* ambapo tunahisi kwamba kazi yake itatusaidia kuangazia masaibu yanayomkumba mwanamke hasa kwa kuyachunguza aliyoandika kuhusu *Nguzo mama*. Bila shaka utata anaouzungumzia ndio utakuwa kwetu darubini ya kuangazia taswira ya mwanamke katika kazi yetu.

Katola (2006) ameshughulikia "*Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili nne.*" Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti ambao ni Muhando, *Hatia* (1972), Mwachofi *Mama Ee* (1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume ni Yahya na Mulwa,*Buriani* (1983) na Mohamed *Kitumbua kimeingia mchanga*, (2000). Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita kwenye misingi ya ubabe-dume. Baadhi ya dhuluma alizotambua ni wanawake kutishwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii miongoni mwa zingine. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Katola ametumia nadharia ya ufeministi wa Kiafrika. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu mtazamo wake kuhusu dhuluma umetupatia mwanga kutambua zile dhuluma kama changamoto ambazo zinaweza kutafutiwa suluhu mwafaka na kupunguzwa kwa sababu haziwezi kukomeshwa kabisa.

Kazi yetu inatofautiana na kazi ya Katola kwa sababu sisi tumetumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ambayo misingi yake imo kwenye mahusiano ya umma, kazi za sanaa na miundo ya jamii. Mwelekeo wetu utatusaidia kugundua ikiwa madai mengine nyeti kama vile 'haki' na 'usawa' yanakubalika kulingana na kaida za kijamii au ni kwa jinsi gani mfumo wa kisheria utasaidia kuinua kiwango cha utekelezwaji. Pia tutajaribu kuchunguza sehemu ambazo dhana ya 'usawa' haiwezi kuwa na uhalisia. Dhana ya usawa kukosekana ni yakinifu kulingana na Honore de Balzac (1799-1850) jinsi alivyonukuliwa na Coser (1963) kuwa:

> *"Usawa ni 'haki' lakini hakuna mamlaka wala nguvu hapa duniani ambayo yanaweza/zinaweza kugeuza dhana hii kuwa ya kweli na halisi".*

Lugano (1989) aliandika na kuonyesha picha ya mwanamke katika siasa na mambo ya kijamii kwa kumulika riwaya za Kezilahabi. Alionyesha kuwa mwanamke anachorwa kama kiumbe anayetegemea mwanaume. Kauli hii ni muhimu kwetu kwa sababu itatusaidia kuchunguza na kubainisha uhalisia wake na athari zinazoibuka kutokana na taswira hii. Mirengo ya nadharia zote za kijamii humulika mifumo ya jamii na katika mfumo wowote ule, kipengele cha utegemezi hakiwezi kukosekana. Kipengele hiki kitatusaidia kuchunguza taswira ya mwanamke kwa kujikita katika tamthilia za waandishi tulizoteua.

Mwita (2005) anasema kuwa, kutokana na mfumo wa kuumeni uliokithiri katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana iliyojaa dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke daima ni mtegemezi. Hali zote za maisha yake hutegemea uamuzi wa mwanamume. Kujiamulia mambo kwa wanawake katika jamii hiyo ni sifa hasi. Anatamatisha kwa kusema kuwa hali hii ni yakini katika jamii nyingi za Kiafrika.

Sisi tunakubliana naye ila kipindi tulicho nacho kwa sasa hali imebadilika. Kipindi cha miaka ya nyuma hali ilikuwa jinsi Mwita anavyoeleza. Mabadiliko tunayoyashuhudia sasa yameletwa na maendeleo ya elimu ya mtoto msichana na uhamasishaji unaoendelezwa na wanaharakati wakisaidiana na baadhi ya wafuasi wa madhehebu ya kikristo. Pia mashirika yasiyo ya kiserikali yametoa na yanaendelea kutoa mchango kuhusu uhamasishaji wa umma juu ya maswala yanayowahusu wanawake. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu itatusaidia katika uchambuzi na uhakiki wa kazi za Muhando na Mwachofi huku tukiangazia taswira ya mwanamke. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na yetu kwa kuwa uchunguzi wake ni kuhusu *"dhima ya ichingero za Wakuria katika kusawiri taswira ya mwanamke"*.na uchunguzi wetu ni kuhusu "*taswira ya mwanamke katika tamthilia ya Nguzo Mama na Mama Ee*".Uchunguzi wake ulikuwa wa nyanjani na wetu umetumia matini za tamthilia.

Matundura Enock (2007) katika tasnifu yake kuhusu "*Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto,*" anasema kuwa mkabala wa kiuana unajishughulisha na maswala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano yanajibainisha katika misingi mbalimbali kama vile kijinsia, kitamaduni, kiutendi kazi, kiu-asasi. Pia ametumia mkabala wa nadharia ya ufeministi ambao ni mkusanyiko wa 'nadharia' nyingi ambao kimsingi lengo lake ni kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu tumepata mambo muhimu ambayo tunafikiri yatajitokeza katika kazi yetu ili kuangazia taswira ya mwanamke. Vipengele hivyo vitatusaidia kuchunguza mwelekeo ambao baadhi ya jamii huegemea na kuibua taswira mbalimbali za mwanamke. Matundura pia amefafanua dhana za uana na jinsia. Amesema kuwa 'jinsia' ni dhana ya kibayolojia na 'uana' ni dhana ya kitamaduni. Dhana hizi mbili zitatusaidia kuangazia taswira ya mwanamke kwa misingi hiyo. Ugavi wa majukumu hufanywa

kuegemea dhana hizi mbili. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu amechunguza taswira dumifu za uana katika *Msichana mlemavu na ndugu zake, Mwanasesere wa Mosi* na *Mgomba changaraweni*. Pia ameangazia taswira dumifu katika *Ndoto ya Riziki, Siku ya wajinga* na *Alitoroka kwao.*

Kitali (2011) ameshughulikia fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* na *Mama Ee*. Kuhusu tamthilia ya *Pango,* anasema kuwa, tatizo kuu linahusu siasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na usasa. Kuhusu tamthilia ya *Mama ee,* anasema ni mchezo unaoyasawiri matatizo yanayoikumba ndoa ya Mwavita na mumewe Kinaya. Pia ameangazia mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, taasubi ya kiume na ubabedume ambao umejikita katika jamii. Sisi tutashughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia mbili ambazo ni *Nguzo Mama* na *Mama Ee.*

Tutajaribu kuchunguza jinsi waandishi Muhando na Mwachofi walivyowasawiri wahusika wakuu kama mashujaa wa kupigania haki zao bila kufanikiwa. Hata hivyo kazi za waandishi hao zitaendelea kuchunguzwa kama kichocheo cha wanaharakati wa kupigania haki za wanawake.

Mirikau (2011) alishughulikia *taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila*. Katika kazi hiyo , Mirikau amejitahidi sana kufafanua istilahi “taswira” kwamba, ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Anaendelea kueleza kuwa picha hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayopitikia akilini mwa binadamu. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Mwanamke anatendewa na hata mwenyewe huweza kujitendea mambo ya kushangaza katika jamii husika. Anatamatisha kwa kusema kuwa, taswira hii ni kuhusu ngazi katika jamii ambayo mwanamke

hujikuta amewekwa na kukubaliana na uamuzi huo unaomfanya aidha atukuzwe au adhalilishwe na hata kujidhalilisha mwenyewe.

Waandishi wa tamthilia tulizoteua ni wa jinsia moja na kazi zao zina ukuruba mwingi. Mawazo ya Mirikau yatatusaidia kuchunguza tamthilia zetu teule ili kuyafikia malengo yetu kwa kumulika matendo anayotendewa mwanamke na kubainisha changamoto zinazomkabili katika mfumo wa kijamii.

Nguta (2011) ameangazia *fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Pango na Mama Ee*. Kazi yake ni muhimu kwetu kwa kuwa yeye ameangazia 'fani' na vipengele vyake vyote. Sisi pia tutajikita katika tamthilia ya *Mama Ee* kwa upande mmoja na *Nguzo Mama* kwa upande mwingine, tofauti na Nguta. Waandishi wa tamthilia alizoteua ni wa jinsia tofauti ilhali tuliowateua ni wa jinsia moja (kike). Nguta ametumia nadharia mbili ambazo ni urasimu (ufani) na ile ya ufeministi. Sisi tutatumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

Kwa mukhutasari,kazi ya Nguta imeangazia baadhi ya vipengele tunavyodhamiria kuangazia hivyo basi kutunufaisha kwa njia moja au nyingine hasa pale wahusika wameangaziwa jinsi wanavyotumia lugha katika mazungumzo baina yao na uzungumzi nafsia (balagha).

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wamezungumzia juu ya 'jinsia' na 'uana' katika kitabu chao *Isimu Jamii* kama vigezo vinavyotumiwa na jamii kuleta ubaguzi. Dhana ya 'uana' ni kigezo cha maumbile ambapo kibayolojia inadhihirisha kama mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume na hali hii haibadiliki kamwe. Kwa upande mwingine uana ni dhana ya kisosholijia ambayo imezalika kutokana na nadharia ya ufeministi inayodai kuwa kijamii mwanamke na

mwanamume wanayo majukumu tofauti tofauti. Suala la dhana ya uana ni tata mno kwa kuwa ni suala lililo na misingi ya kijamii au kisosholojia. Kwa mfano, mtoto anapozaliwa hupewa jina na hilo jina litatambulisha jinsia yake.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

Tulisoma kwa kina vitabu tulivyoviteua-*Nguzo Mama* na *Mama Ee* na kugundua maswala yaliyoibuliwa na waandishi hawa, Muhando na Mwachofi. Pia tulisoma na kuchunguza tasnifu zenye uhusiano na somo letu pamoja na matini zilizopatikana katika maktaba. Pia tutachunguza makala ambayo yanaweza kutupatia mchango wa mawazo kuhusu mada hii. Tutafanya uchunguzi wetu kwa kutumia tarakilishi ambazo zitatusaidia kufanya upekuzi kutoka kwa mtandao. Utafiti stahilifu utatufaa kwa kazi hii kwa sababu malengo yetu ni kuchunguza na kubainisha changamoto zinazochangia wanawake kutofaulu kupata haki wanazodai, jinsi baadhi ya waandishi wamewasawiri wanawake kikamilifu ili kudhihirisha uhodari wao na majukumu wanayopewa wanawake kupitia asasi za kijamii yanavyochangia kutopatikana mafanikio katika harakati zao.

## 1.10 HITIMISHO

Mada yetu ya utafiti inahusu "taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee."* Waandishi wa tamthilia hizi ni wa jinsia ya kike na kila mmoja aliandika kazi yake kipindi tofauti ili kusheheni mambo yanayozikumba jamii zao kupitia mifumo ya asasi za kijamii.

Uchunguzi wa maswala yanayowakumba wanawake haujafanywa kwa wingi kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi na migogoro inayopatikana kwenye tamthilia hizi ni kielelezo

cha yale yanayopatikana katika jamii za waandishi. Maswala haya yanaendelea kuangaziwa na waandishi na wahakiki wa fasihi.

Malengo ya utafiti wetu yamekuwa: kuonyesha jinsi baadhi ya waandishi wamewasawiri wanawake kama mashujaa, kubainisha kuwa majukumu anayopewa mwanamke kupitia asasi za kijamii yanachangia sana mwanamke kutopata mafanikio katika harakati zake na kubainisha jinsi changamoto zinazowakabili wanawake zimechangia kutofaulu kupata haki zao.

Katika baadhi ya kazi za kifasihi, aghalabu mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu, mnyonge, mwongo na chombo kisichothaminika miongoni mwa chukulizi zingine. Hii ndiyo sababu kuu iliyotupatia msukumo kuangazia kinachosababisha mitazamo hii miongoni mwa baadhi ya waandishi. Utafiti wetu utakuwa wa usomaji maktabani ili kukusanya data ya kuchambua, kutathmini na kutolea kauli. Tumepitia yaliyoandikwa kuhusu mada tukayalinganisha na kuyalinganua ili kutupatia mwelekeo wa kazi yetu. Nadharia ambayo tumetumia kama darubini ya uchunguzi wetu ni Sosholojia ya Fasihi ambayo imo miongoni mwa nadharia za kijamii. Hatua hii inaturuhusu kuingia sura ya pili ambapo tutashughulikia uchambuzi na uhakiki wa tamthilia ya *Mama Ee.*

# SURA YA PILI

# UCHAMBUZI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA YA MAMA EE.

## 2.0 UTANGULIZI

Mtoto anapozaliwa bila shaka lazima alie. Anakua akinung'unika na anpokuwa mmtu mzima yamkini huaga dunia kabla hajatosheka. Kwenye utangulizi wa *Mama Ee* tunapata wanawake watatu.Wa kwanza ni binti mwenye umri wa miaka kumi na sita, na ni mjamzito, amevaa matambara na amejitwika mikono kichwani huku akilia. Picha tuliyoipata inadhihirisha mazingira ya kukosa tumaini na hali ya umaskini.Mwanamke wa pili ilisemekana kuwa alikuwa amevalia vizuri, amebeba mtoto mgongoni lakini pia alikuwa akilia kwa uchungu, kuashiria kuwa ana mambo yanayomhangaisha kisaikolojia licha ya kuwa na uwezo. Mwanamke wa tatu alikuwa amebeba mtoto mgongoni, kitambaa kikuu begani na tita la kuni kichwani. Hii ilituonyesha taswira ya mwanamke miongoni mwa jamii nyingi zenye utamaduni wa Kiafrika.

Tulishughulikia baadhi ya vipengele vya fani kama vile wahusika, mazingira na vipengele vya maudhui na dhamira. Somo hili linaafikiana na wataalamu ya kuwa fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa kuwasilisha maudhui. Nyenzo hizo ni muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Hatutashughulikia vipengele vyote vya fani isipokuwa vipengele vya wahusika na mandhari. Maudhui nayo ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Tulishughulikia vipengele vyote vya maudhui ambavyo ni dhamira, ujumbe, mtazamo, msimamo, falsafa na itikadi kama tutakapobainisha baadaye.

*Mama Ee* ni tamthilia ya masaibu katika ndoa ya Mwavita  na Kinaya. Mwavita aliolewa kisha akatumbukia kwenye lindi la matatizo yanayopatikana kwenye baadhi ya ndoa nyingi katika jamii zetu. Pia ni kilio cha Tenge dadake  Mwavita aliyekuwa amepachikwa mimba na George, jambo lililosababisha kutimuliwa kwa Tenge kutoka shuleni.

Mwandishi alitumia shairi la tarbia katika utangulizi wa kazi yake. Shairi hili ni ngonjera na pia aliwatumia wanawake hawa watatu akidhamiria kutuonyesha kuwa duniani kuna matabaka ya wenye nguvu na wanyonge. Tabaka la wanyonge linajipa moyo wa subira, kutia juhudi na kupinga unyonyaji, kutafuta uhuru, kuungana kudai haki, kujitegemea na kukataa kutwikwa majukumu kupita kiasi, kugandamizwa, kupuuzwa na kupigwa.

## 2.1 MATATIZO YA UNYUMBA

Matatizo ya unyumba ni sehemu ya maisha kwani yana uzuri na ubaya ambao wahusika wakiutathmini kwa mtazamo chanya, watapiga maendeleo ya kuwa na familia zenye mshikamano. Tunasema hivyo kwa sababu kila mmoja atagundua kile mwenzake hapendi na kujaribu kukiepuka. Hata hivyo matatizo ya unyumba yakizidi kiasi kisichoweza kuvumiliwa, kutakuwa na athari mbaya itakayosababisha familia kukosa mapenzi na mshikamano thabiti. Kulingana na kauli hii tunaangazia maisha baina ya Mwavita na Kinaya wakiwa mjini kwenye makazi yao na walikofanya kazi.

Mwenye nyumba, alifahamu kuwa Kinaya ndiye mpangaji wake lakini hakufahamu kuwa Kinaya alikuwa ameshamtwika mkewe Mwavita majukumu yote ya kuitunza na kuikuza familia yake. Kinaya hakuwa na habari jinsi kodi ilivyokuwa ikilipwa wala chakula kilivyokuwa kikitafutwa nyumbani. Kuna dhana miongoni mwa baadhi ya jamii ya kuwa ikiwa bwana

yungali hai, mkewe hawezi kuwa mumiliki wala kuhesabiwa kuwa ana chochote.Mwavita alipenda kulalamika kwa sababu ya masaibu aliyokuwa akipitia katika ndoa yao.

Baada ya kuolewa na Kinaya, walibahatika kupata mtoto waliyemwita Juma. Malezi ya watoto wachanga ni magumu sana kwa sababu ni kiumbe kisichoweza kuwasiliana kwa urahisi. Wazazi wanagenzi huwa hawana uzoefu wa malezi ya watoto wachanga. Hii ndiyo hali iliyomkumba Mwavita. Shida ya ugonjwa wa Juma ilimletea Mwavita msongo mpaka akaanza kujilaumu na kujihisi kama mnyonge, hata ikamlazimu kutafuta msaada wa wauguzi wa kumhudumia Juma bila msaada wa mumewe. Juhudi za kumsaka Kinaya siku nzima ziliambulia patupu. Kinaya alirejea nyumbani saa tisa za usiku na kumuamrisha Mwavita afungue mlango haraka iwezekanavyo lau sivyo angelitupwa nje. Baada ya mlango kufunguliwa, majibizano yalizidi na ugomvi kutokea ambao hatima yake ni Mwavita kupigwa na kung'olewa meno. Mabishano yalitangulizwa kwa stihizai na Kinaya kama ifuatavyo:

> **KINAYA**: *"Jike gani hili nililiowa! Kunifungulia mlango taabu na hata niingiapo anitazama kama niliyetapakaa mavi! Ulikuwa na nani hapa ndani nilipoanza kubisha? Ee? Sasa umekasirikia nani? Ee? Ni nini sasa? Una nini?"* (*Akamsukuma kwa nguvu*).
>
> **MWAVITA**: *"Sina lolote nakuona wewe unayenishukia kwa vishindo saa tisa za usiku au asubuhi bila kuniuliza hali! Mmh! Kinaya we! Kumbe ile "I love you-nakupenda Mwavita" ndipo ilipoishia kabla ya miaka mitatu kuisha! Loo!" Uk. 3.*

Hii ndiyo hali ambayo huwakumba baadhi ya waliooana. Aghalabu ni vigumu kubaini dosari za mwenzako kabla hamjaingia kwenye uhusiano wa kindoa. Wahusika huwa wanajitahidi iwezekanavyo kuficha kasoro hizo ingawaje mara nyingine dosari zao huweza kufichuka kupitia

kwa watu wengine. Hali hii inafananishwa na mtu anayetaka kumweka ng'ombe kamba muguuni. Ni lazima aifiche ile kamba hadi pale itawekwa mguuni. Katika hali halisi ya ndoa, ni vigumu sana mvulana au msichana aweze kugundua tabia ya mwingine kikamilifu kabla ya ndoa. Baada ya ndoa ndipo wanandoa hujuana kisawasawa.Ndoa huwalazimu wahusika kukabiliana na hali halisi kuhusiana na wenzao.

Majina ya wanandoa hawa ni ya kimajazi. Kinaya alilalamika kuwa mamake Mwavita alifahamu vizuri kuwa jina lenyewe latosha kumjulisha mtu tabia yake ndiposa Kinaya akasema,

> **KINAYA**: *"Mwavita! Nawe u Mwavita kweli. Lete chakula haraka uondoe tabia uliyofunzwa na mamako hapa! mababu zetu hawakulazimika kulipa pesa zaidi ati kwa kuwa mke ana shahada! Akina baba siku hizi wanawauza mabinti. Mimi nililipa shilingi elfu mbili zaidi kwa kuwa ulifika kidato cha sita."*

Kinaya alifikiri kuwa Mwavita alileta ukinzani kwa sababu alipata ajira iliyomfanya awe na mapato yake. Sababu hii ilisababisha Kinaya kuwaendea waajiri wa Mwavita na kuwarai kuwa wamfute Mwavita kazi jambo ambalo lilipata pingamizi kali kutoka kwa mwajiri wake kwa sababu ya uwajibikaji wake na huduma nzuri aliyokuwa akiitoa. Pingamizi hizo zilimfanya Kinaya kufikiri kuwa Mwavita alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwajiri wake. Mwavita alimweleza Kinaya kuwa, sio watu wote ambao hushiriki usherati makazini mwao. Mwavita alimwambia Kinaya kuwa, azurure lakini asije akamwambukiza magonjwa ya zinaa. Pia Mwavita alimsihi Kinaya kuwa asiingilie kazi yake maana kazi hiyo ilikuwa mbadala wa bwana, ilikuwa inalipa pesa za kukidhi kila hitaji la nyumbani-chakula, nguo, mtoto kila kitu. (Uk.6.)

Baada ya hayo Kinaya alidhamiria kumwamsha Juma ambaye alikuwa amelala mda kitambo kidogo tu baada ya kumhangaisha mamaye siku nzima. Kwa sababu ya yale masaibu Mwavita

alikuwa ameyapitia mchana na karibu usiku kucha, alimkataza mumewe kumwamsha mtoto lakini Kinaya alitumia nguvu na mamlaka jambo lililodhihirisha madharau kwa mkewe na kutojali kwake. Baada ya mvutano Kinaya alimwambia Mwavita kuwa:

> **KINAYA**: *"Nina hakika kuwa Juma ni mwanangu ila sina hakika ya mtoto aliye tumboni"*.

Taswira tunayopata hapa kutokana na dai hili ni kwamba Mwavita ni mwasherati ambavyo sivyo. Kinaya alimdhania mkewe alikuwa amebadilisha mwenendo wa maadili yake akiwa na lengo la kulipiza kisasi. ( Uk.7.) Kumshuku mtu kwa jambo lolote pasina ushahidi wowote huleta hali ya kutoelewana na kuharibu mahusiano. Kinachoathiriwa kwa hali kama hiyo ni mawasiliano baina ya mshuku na mshukiwa. Shutuma za Kinaya zilimfanya Mwavita kusema kwamba:

> **MWAVITA**: *"Juma ni mtoto wako kwa kuwa ulijifurahisha kwangu. Hilo tu, ndilo linamfanya Juma anakuwa mwanako". (Uk.8.)*

Kama hazingekuwa juhudi na mshahara wa Mwavita, Juma angekuwa ameishaiaga dunia kitambo. Mwavita alidhani kuwa dhamira ya Kinaya ilikuwa kumwachisha kazi na kumlemaza kiuchumi ili Kinaya awe na uhuru wa kufuatana na mahawara zake mjini. Baada ya Kinaya kufahamishwa na mkewe juu ya wazo hili, Kinaya alimwambia:

> **KINAYA**: *"Hakuna mahawara mjini kuliko dadako Tenge"*.

Usemi huu ulimwuudhi Mwavita mpaka akathubutu kumwambia mumewe kuwa:

> **MWAVITA**: *"Dada zako watatu wanazurura ovyo mjini kama mbwa koko bila mabwana". (UK. 10.)*

Matokeo ya mvutano huu yalikuwa kupigwa kwa Mwavita hadi akang'olewa jino.

Kwa kweli, wanandoa wengi hawahisi vizuri wakati ambapo jamaa zao wanapotajwa kwenye ugomvi usiowahusu. Ni jambo ambalo wanandoa wagombanao hujikuta wameliingiza kwenye ugomvi na linazua chuki na uhasama baina yao. Ugomvi wa Kinaya na mkewe ni kielelezo cha yale yanayopatikana nyanjani katika jamii nyingi za Kiafrika.

Uandishi wa kazi za kifasihi ni shughuli ya kibunifu iliyo na dhima ya kuzindua na kuuhamasisha umma kuhusu masuala ambayo yanatisha kuzisambaratisha jamii na kurudisha nyuma maendeleo. Malezi bora ya watoto yanategemea ushirikiano wa wazazi wote na jamii yote. Hata hivyo kuna baadhi ya familia ambazo furaha hupatikana kipindi kifupi baada ya harusi lakini baadaye misukosuko huanza na kusababisha jitimai. Tuna baadhi ya familia ambazo aghalabu zimejiweza kiuchumi, lakini vita na mafarakano haviishi, malumbano yamekuwa kawaida ya maisha. Miongoni mwa baadhi ya familia, baba anapoingia nyumbani huku akipiga kelele na kuamrisha kila mtu kwenye boma, watoto na mama hutoroka kwa kupitia mlango wa nyuma au dirishani. Athari zimekuwa nyingi kwa sababu ya maisha ya aina hii. Kwa mfano, watoto wanafundishwa uhasama dhidi ya mzazi, kina mama wanapigwa na kulemazwa, wengine wanauawa na baadhi wanatoroka na kutafuta hifadhi kwingineko huku wakiwaacha watoto wakiteseka na kuhangaika maishani.

Katika tamthilia ya *Mama Ee* Juma aliachwa na mamake baada ya talaka baina ya wazazi wake. Kina mama wengi wameamua kuvumilia masaibu mengi kwa sababu ya watoto. Upendo na huruma kwa ajili ya watoto, ni kamba zinazowafunga baadhi ya wanawake na kuwazuia kuhama makwao. Wengine huhofishwa na majukumu ya malezi pindi waondokako kwa waume zao. Pia wanaume wengi hawawezi kumchukuwa mwanamke ambaye ana watoto waliozaliwa kwa mume

mwingine. Kuna baadhi ya jamii ambazo haziwezi kumruhusu mwanamke aliye na watoto wa mume mwingine kuingia na hao watoto kwenye boma lao, ni mwiko. Juma aliachwa na mamaye baada ya kuvumilia kwa kipindi kirefu masaibu yaliyomkumba kwenye ndoa yao. Mwishowe mama mzazi na dadake Mwavita, walimshawishi Mwavita kurudi kwa Kinaya na kumlea mwanaye kwa maana kama angekosa kurudi, Kinaya ataoa mke mwingine na Juma kuishia kukulia katika mikono ya mama wa kambo.

Ushawishi huu ulimfanya Mwavita kurudi kwa Kinaya. Aliporudi na kukaa kipindi fulani, aliweza kupata mimba ambayo ilimfanya kupitia kipindi kigumu cha kuhisi uchungu na maumivu mengi. Alipokuwa akila chochote au hata kumeza dawa, alilazimishwa na hali hiyo kutapika. Mahangaiko haya yalimfanya Mwavita kujuta na kujilaumu kwa kusema:

> **MWAVTA:***"mimi niliingia kivulini kwelikweli! Sijui ni nani aliyetunga sheria ya watu kuoana-Balaa tupu!"(Uk.59)*

Tenge kwa uzoefu wake akamwambia dadake kuwa, asipoolewa atazaa wanaharamu kama yeye, aitwe hawara na kila mtu, wake kwa waume. Mazungumzo baina ya Tenge na Mwavita yalidhihirisha kuwa msichana akipata mimba na kujifungua kabla hajaolewa, hastahili kupata heshima kutoka kwa jamii ingawa kwa sasa jamii nyingi zimehamasishwa na kulegeza msimamo huo.

Mawazo ya wahusika hawa kuhusu muundo wa jamii yanalenga swala la kimsingi ambalo linaweza kuchunguzwa kwa kutummia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Ili kuyatetea mawazo yake, Mwavita alieleza kuwa, heshima haina manufaa kwa mtu ikiwa mtu huyo atakosa uhuru wa kutenda jinsi apendavyo. Kila afanyalo lazima likubaliwe na mume. Kauli hii ilitajwa na

Mwita (2005) alipokuwa akifanya utafiti wake kwamba, “hali zote za maisha ya mwanamke hutegemea uamuzi wa mwanamume”.

Baada ya mda mfupi Kinaya alirudi na kumkuta Mwavita akiwa katika hali mbaya. Harufu kutoka kwa Kinaya ilimzidishia Mwavita matatizo. Kinaya alijikuta kwenye mtanziko. Akitoka ni lawama. Akirudi nyumbani ni lawama. Hakujua afanye nini. Alitakiwa aende sherehe na akahoji kuwa wenzake wote watakuwa na wake zao shereheni kwa hivyo jambo hili likamtatiza. Akihudhuria bila kuambatana na mkewe ataonekana kama mtu ambaye hajaoa na hii itamletea aibu. (Uk.65.) Kinaya alipogundua kuwa nguo zake za kwendea sherehe hazikuwa zimepigwa pasi alijipata mashakani akaanza ugomvi na vita huku akiropoka maneno yaliyomkwaza Mwavita na Tenge. Aliporomosha matusi chungu nzima kisha akamwamrisha Tenge kuondoka kwake pamoja na mwanawe. Kinaya alimfananisha Tenge na joka kubwa la balaa. (Uk.67.) Mwenendo huu wa Kinaya ulimkasirisha sana mkewe hasa kwa kudai yeye na Tenge kuwa wanawake wawili waliomo nyumbani kwake wasio na shughuli muhimu isipokuwa kuchunguza maisha yake!

Baada ya vurumai, Mwavita na Tenge waliamua kuondoka na kumwachia Kinaya nyumba aliyodai kuwa ni yake ilhali hakuwa akiilipia kodi wala kutoa chochote kilichokuwa kikiliwa mle.

Hiki ni kielelezo cha jinsi familia nyingi zinavyoshuhudia mafarakano yanayowahusisha jamaa na baadhi ya wanafamilia wengine kulingana na misimamo, falsafa na itikadi zao. Hasa mashemeji wanachukuwa nafasi ya kwanza katika lawama na chanzo cha ndoa nyingi kusambaratika. Jamii zetu zinakumbwa na matatizo ambayo kwa kweli hayawezi kubainishwa ya kwamba yanasababishwa na jinsia moja dhidi ya nyingine. Hata kuna baadhi ya wanaume

ambao hudhulumiwa na wanawake. Ni muhimu kutambua dhuluma inaweza kuainishwa kuwili na itategemea ni nani anaye mdhulumu mwingine.

## 2.2 UBAGUZI WA KIJANA WA JINSIA YA KIKE

Swala la ubaguzi ni nyeti na linazua matatizo mengi katika jamii zetu. Ubaguzi hujikita katika misingi mbalimbali kama vile jinsia, ukabila, rangi, umri, kitaaluma na maumbile miongoni mwa mingine. Hali hii ilimkumba Tenge aliyekuwa amepewa ushauri nasaha na mama yake akiwa mtoto mdogo ya kwamba asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Babake Tenge ni mzazi aliyekuwa na tabia ya ubabe-dume. Pia kakake Tenge alifanana na babake kitabia. Kwa bahati mbaya Tenge alipachikwa mimba na George kisha yeye akafukuzwa shule naye George akabaki shuleni na kuendelea na masomo yake. Matukio kama haya yanamulikwa vyema na nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi kwa sababu baadhi ya vipengele ambavyo nadharia hii inashughulikia ni muundo wa jamii. Tukio hili ni dhihirisho la jinsi taasisi zetu za kijamii zinavyoendeleza ubaguzi. Mbona George hakufukuzwa shule!

Tenge alipofika nyumbani alianza kulia kwa sababu ya mimba ambayo alikuwa ameipata. Alifahamu baba yake alikuwa mkali mno na hakuwa na huruma. Tenge alimlilia mama na kumwomba msamaha hata kabla hajamjulisha kosa alilolifanya. Mama alipogundua kuwa Tenge alikuwa amepachikwa mimba, mama alijuta na kusema:

> **MAMA**: *"Ewe mtoto wa kike-umeniletea balaa na beluwa.*
>
> *Nitafanya nini? Nitaenda wapi? Ole wangu! Najuta kuzaa"( UK.13.)*

Majuto haya ya mamake Tenge ni kielelezo cha matatizo yanayowakumba baadhi ya wanawsake katika familia zao pindi tu binti zao wanapopata mimba kabla ya ndoa. Visa vya watoto wa kike

kupachikwa mimba vimeongezeka kwa kwa sababu ya mfumo wa kijamii ambao umechukua mkondo mwingine tofauti na ule wa kitamaduni. Tenge alimsihi mama kuwa amsamehe na akadai kuwa George alimdanganya na alikosa mara moja tu. Lakini maji yakishamwagika hayazoleki. Hata kama alikosa mara moja, ameathirika. Wahenga walisema majuto ni mjukuu na sasa Tenge alikuwa taabani na majuto yalimwandama.

Jambo la kushangaza hapa ni kwamba, wakati nduguye Tenge alipowapachika wasichana watatu mimba, mamake hakuwa na wasiwasi. Lakini wakati binti wake alipopatwa na shida kama ile iliyowapata wale mabinti wengine, alilia na kuhuzunika sana. Kweli waliosema kuwa mkuki kwa nguruwe ni mtamu, lakini kwa binadamu ni mchungu hawakukosea. Baba alipogundua kuwa Tenge amepata mimba, alimlaumu mama kana kwamba alijua chanzo cha shida hii. Alimlaumu mama kwa kutodhibiti mienendo ya mabinti zake. Baba alichukuwa fimbo akaanza kumchapa Tenge na kumwamuru aondoe aibu yake kijijini. Mama alipojaribu kumkataza mumewe a kampiga Tenge, kakake Tenge aliingilia na wakashirikiana na babaye kumwadhibu Tenge.

Tenge naye alijikaza na kumsuta nduguye kuwa amewahi kuwatia mimba takribani wasichana watatu lakini yeye hakuchapwa wala hakuulizwa na mtu kwa nia ya kufukuzwa kutoka nyumbani au kuadhibiwa. Tenge alilalamika kwamba yeye anaadhibiwa kwa kosa kama la nduguye ambaye hasemeshwi wala kuadhibiwa. Alidai kuwa:

> **TENGE**: *“Lakini mama kwa nini mimi tu nataabika? Nimefukuzwa shuleni,yeye George aelimika? Kosa letu, hadharani mimi tu meumbulika, kweli dunia ya wawi, duni ya waume.”( UK.18)*

*“Kaka anipigiani? Anitesa anioneya kwani hapa kijijini watatu mimba ‘mewatiya. Hakufukuzwa nyumbani, hakurai hakutubiya”. (UK. 19.)*

Wanawake ni wanyonge. Tuligundua kuwa katika onyesho hili kulikuwepo na ukosefu wa haki. Katika maamuzi mengi ya kijamii kuna hali ya kuonea na kuegemea upande mmoja. Hili ni swala ambalo linafaa liangaliwe kwa mtazamo mpya na kwa tahadhari zaidi. Maana si vyema watu wawili au makundi mawili yafanye kosa kwa kushirikiana, moja lilaumiwe na lingine lisilaumiwe. Kwa mfano, George na Tenge walishiriki ngono. Baada ya Tenge kupachikwa mimba, yeye akafukuzwa shuleni, George akabaki akiendelea na masomo, jambo ambalo linadhihirisha ubaguzi na upendeleo. Kaka yake Tenge aliwatia mimba wasichana watatu, yeye hakuulizwa wala kuchapwa na kuamrishwa kuondoka kijijini. Tenge alipopachikwa mimba alipigwa na kuamrishwa kuondoa aibu kijijini.

Haya ni baadhi ya matatizo yanayowakabili baadhi ya wanajamii wa jinsia ya kike. Mwanamume akifumaniwa na mke wa mtu mwingine, mke huyu atalaumiwa na hata kutusiwa, lakini ni bayana kwamba mwanamke hawezi kufanya shughuli hiyo ya umalaya bila ya mwanaume kuwepo.

## 2.3 NAFASI YA MILA NA DESTURI KATIKA NDOA

Mila ni istilahi inayomaanisha jumla ya maisha ya jamii mahsusi. Kila jamii ina kanuni zinazoiongoza na kuhakiki upendo, utangamano na umoja vimedumishwa kwa ajili ya maendeleo na ukuaji. Kulingana na jinsi hali ilivyokuwa, familia ya kinaya walikwenda kwa mzee Tembo kutafuta suluhu baina ya Mwavita na Kinaya ambao walikuwa wametengana kwa sababu ya ugomvi wa kiunyumba ambao ulikithiri nyumbani kwao. Matatizo mengi yaliibuka kwa sababu Kinaya na Mwavita hawakuelewa kaida za kimila walizohitaji kuzingatia. Wawili

hao walilaumiwa kwa sababu ya elimu ya kimagharibi ambayo ilikuwa imewafanya wasahau mila na desturi yao. Tulimpata nyanyake Mwavita akijitokeza na kudai kuwa kazi ambazo wanawake wanazoziona kuwa ni nyingi, walizitaka wenyewe. Alianza kwa kueleza kuwa:

> **NYANYA**: *"Kazi hizo wanawake walizitaka wenyewe. Zamani za kuumbwa mwanadamu, Mungu aliwagawanyia watu kazi-za wake na za waume. Hakufanya hivyo bila kuwauliza babu na nyanya zetu wa kwanza wangependa kazi zipi. Basi Mungu aliwauliza nani atakayebeba mimba na kuzaa watoto-mke akamkatiza na kujibu kwa sauti-"ni mimi", akauliza tena-nani atakayepika chakula na kufanya kazi zote za nyumbani-mke akadakia tena kwa sauti "mimi". Kazi zote alizitaja Mungu mke akasema atafanya yeye. Mume alinyamaza maana hakuwa na ulimi mwepesi kama wa mke. Mungu aliuliza, "Nani atakayekuwa mwindaji?" Mume akajibu kwa sauti ya chini, "mimi". Ndiyo maana mke ana kazi nyingi zaidi, ulimi wake ulimchongea!" (UK.24).*

Kilichozua usimulizi huu wa nyanya ni lawama iliyokuwa imetolewa na mzee Tembo kuwa wageni walikuwa wamewekwa kwa mda mrefu bila kupatiwa hata chai. (Uk.23.) Mjadala uliendelea kwa muda mfupi kisha wakaingilia swala lililokuwa limewakutanisha –kutengana kwa Mwavita na Kinaya. Mzee wa kijiji ndiye aliitwa na kupewa uwenyekiti wa kikao cha siku hiyo.

Bamkubwa wa Mwavita alidai kuwa Kinaya alifanya makosa kwa kwenda kwa wakwe akiwa mlevi, kuwatukana baba wakwe washenzi, kumsukuma na kumtukana Mwavita mbele yake. Mzee wa kijiji aliwatahadharisha kuwa wasiwashe moto na kuuchochea ila wajaribu kuuzuia kwa kujizuia na kuondoa hasira maana 'hasira ni hasara'.Nyanya alisimulia jinsi sheria za

zamani zilivyowaongoza kutunza na kuonyesha heshima kwa wazazi wa mke wa mtu kwa kusema:

> **NYANYA**: *"Wakati unapomsalimu mama au baba mkwe humshiki mkono. Hayo yote ni kwa sababu inatakikana heshima mbele yake." (UK.30.)*

Kwa muktadha huu ilimbidi Kinaya kuhakikisha kuwa asile au kupita mbele ya mama mkwe au kumgusa. Waathiriwa Kinaya na Mwavita walihojiwa kuhusu chanzo cha ndoa yao kukosa amani na kila mmoja akatoa yote yaliyokuwa moyoni. Katika kikao hicho, Kinaya alipatikana na makosa mengi. Baadhi ya makosa yake yalikuwa ulevi na kutofanya kazi ili aikimu jamii yake.

Mwavita aliwaeleza wazee kuwa ulevi wa Kinaya ndicho kiini kilichokuwa kikisababisha ukosefu wa amani nyumbani mwao. Pili, mumewe alikuwa na mazoea ya kufika nyumbani usiku wa manane jambo ambalo lilimfanya Mwavita akose usingizi akimsubiri. Wakati mwingine hasa mwisho wa mwezi siku mbili zingeweza kupita bila Kinaya kuonekana nyumbani.

Baba mkubwa wa Mwavita alieleza kikao kuwa wao zamani walioa wake lakini siku hizi watu wananunua watumwa na kuwafanya ngoma wawe wakipiga watu wasikilize mlio. Kinaya alidai kuwa Mwavita alikuwa akimnyima chakula. Dai hili lilimshangaza nyanyake Mwavita na kumfanya aulize kwamba:

> **NYANYA:** *"Mwavita somo, kwa nini kumnyima mumeo chakula?* Na kumshauri kuwa: *Hiyo ilikuwa kazi yake. Kumpikia bwanako na wanao. Hata kama mlevi namna gani lazima umpe chakula". Uk.46.*

Ilibainika kuwa wakati mwingine Mwavita akiwa mja mzito, Kinaya alikuwa na mazoea ya kumlazimisha kuamka usiku wa manane ili ampikie. Babake Kinaya akamshauri mwanawe kuwa:

> **BABAKE KINAYA**: *"mke mja mzito husaidiwa kazi sio kuongezewa kazi ya kupika mara mbili usiku wa manane. Hata akianza ugomvi mume hunyamaza na kutafuta mbinu ya kuepuka kwa kuondoka akaenda matembezi. Pia ajue kuwa wakati huo si mke anayesema ila shetani wake amtumaye kutukana, lazima mume astahimili kipindi hicho." (Uk.47-48.)*

Kikao kiligundua kuwa makosa yaliyokuwa yakifanywa na wanandoa hawa yalitokana na malezi ya wazazi wao. Mwavita alishauriwa arudi kwa mumewe lakini akasema kuwa:

> **MWAVITA**: *"Mtu hamwoni nyoka mwenye sumu, aliyemuuma siku moja akarudi tena kumkanyaga". (Uk.49.)*

Lakini mwenyekiti akamshauri Mwavita kuwa lazima amfikirie mwanawe Juma. Mwenyekiti, alimwona mtoto Juma kama kikazandoa au kamba inayomfunga Mwavita kwa mumewe. Alichosahau ni masaibu aliyokuwa akiyapitia Mwavita kama vile kuachiwa majukumu ya nyumbani, kupigwa na kukesha akimsubiri mumewe usiku kucha miongoni mwa mengine. Mkewe Kinaya alipitia maisha magumu kipindi hicho kulingana na mwenendo wa mumewe. Ndio maana Mwavita alikosa imani kwa mumewe ambaye alionekana kujuta na kuomba msamaha. Mwavita alitetewa na bamkubwa wake akasema kuwa:

> **BA MKUBWA MWAVITA**: *"Huyu bwana mwataka kumpa ngoma yake aende nayo aendelee kupiga aone raha."*

Kikao kiliafikiana kumtoza Kinaya ili ahisi uchungu na kuona makosa yake. Kinaya alisihi kikao kimruhusu mkewe aende naye ili awe akilipa faini polepole kwa awamu lakini akajulishwa kuwa mila na sheria za kitamaduni haziruhusu. (Uk.56.)

Mwishowe mzee wa kijiji ambaye pia alikuwa ameshikilia hatamu za uwenyekiti wa kikao aliwadokezea wanakamati kwamba, mwanamke aliyekataa kurudi kwa bwanake baada ya faini kulipwa alilazimishwa kwa nguvu. Walitumia mbinu kama vile kushawishi lakini mbinu hii ilipokosa kufanya kazi, lazima haikuwa na budi na:

> **MZEE WA KIJIJI**: *"Lazima yenyewe ilikuwa ni kumfunga kidole. (Uk.57.) Bwanake akisha fanya malipo na ashikilie kutorudi kwake, huitwa wazee hasa jamaa zake, wazee hushauriana naye polepole, akikataa katakata, basi huletwa ukamba mwembamba kama uzi lakini thabiti usioweza kukatika. Hushikwa kidole cha shahada cha shoto na kufungwa, hukazwa sana na ukamba huo huvutwa na kufungwa kwenye nguzo ya nyumba. Hukazwa hadi pale atahisi uchungu na kukubali kurudi. (Uk.58.)*

Wengi waliokaidi kutorudi baada ya mbinu hii kutumika waliishia kupoteza vidole vyao. Pia wake wengi walilazimishwa kuolewa kwa vidole na wengine wakawaacha mabwana kabisa licha ya kukatwa vidole. Huu ni ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba mila na deturi za kale ambazo zimepitwa na wakati hazingetumika kumrejesha Mwavita kwa bwanake. Mila na deturi za kale zilikuwa na ukiushi mkubwa wa haki za binadamu na ni mzigo kwa mwanamke.

## 2.4 NAFASI YA DINI KATIKA MAHUSIANO YA KINYUMBA.

Dini ni muhimu sana kiasi kwamba binadamu hawezi kujitenga nayo hata kama ana huo ufahamu au hana. Tunatoa kauli hii kwa sababu kila mtu mwenye akili timamu ana imani juu ya mambo fulani aidha ya kibinafsi au ya umma yanayomfanya kuwa na mitazamo mbalimbali

kuhusu maisha. Pia kuna kanuni na kaida zinazowaongoza watu katika jamii zao mahususi. Kanuni hizi pamoja na miiko ni sehemu ya dini yoyote ile inayopatikana duniani. Tena ni kipengele kinachochunguzwa sana na wanataaluma mbalimbali kama vile wanasosholojia na wanafasihi. Pengine tutakubaliana kwamba mtu anaweza kujitenga na wafuasi wa dini yake kwa kutohudhuria sehemu za ibada lakina hawezi kujitenga kamwe na dini.

Dini ni kipengele muhimu ambacho kinatajwa kama sehemu inayotumika kuwafanya wanawake wakubali kujisalimisha na kudhulumiwa kwa hiari yao. Mamake Mwavita alimtembelea kwenye makazi mapya lakini si kwa sababu ya shughuli za ibada. Mama alifika pale ili kumtuliza mwanawe na kumtia nguvu aweze kustahimili na kuwa mvumilivu kwa kuwa dunia hii ni uwanja wa fujo. Mwavita alikuwa amesongwa na mawazo kwa sababu ya kutengana na bwanake na mwanawe Juma ambaye bado alikuwa akihitaji malezi ya mama mzazi. Baada ya mazungumzo yao, Mwavita aliwaza na kusema:

> **MWAVITA:** *"Wanawake wataendelea kunyonywa na kunyanyaswa na mabwana kwa kutojua haki zao. Wengi washakubali kuwa wananchi wa tabaka la chini. Ati ndivyo Mungu alivyotuumba. Wanawake kama hao huwachukuwa waume kama miungu. Mtu kama mimi huchukuliwa kama mwasi. Nimeasi dini gani? Kuabudu waume. Simwabudu mume yoyote!" (Uk.77-78.)*

Baadhi ya wanawake wengi waliosoma wana mawazo kama haya ya Mwavita na mwonoulimwengu wao ni tofauti, ndiposa Mwavita akasema kuwa:

**MWAVITA:** *"Nimegundua kuwa hasimu yangu si mume tu bali pia mke, mwabudu mume. Huyo ndiye hasimu mkuu mno. Atanitafutia kila aina ya tusi kwa kuwa nimeasi dini yake".*

Walipokuwa wakiendelea na mazungumzo, padre aliingia na kumshukuru Mungu kwa kuwa alimkuta mamaye Mwavita. Padre alimweleza mama kwa kifupi jinsi alikuwa ametia juhudi za kuwapatanisha Kinaya na mkewe bila kufanikiwa. Padre alishambuliwa na Tenge kwa sababu walikuwa wakishirikiana na Kinaya ulevini. Tenge alimkemea na kumwambia:

**TENGE**: *"Kwenda zako na kanisa na sakramenti zako. Kudanganya watu tu".*

Ilibidi mama aingilie kati  na kumnyamazisha Tenge. Kisha mama alitaka kufahamishwa ikiwa padre alikuwa na mke. Padre alijibu kuwa, hakuwa na mke ndiposa Mwavita akapata nafasi ya kumshambulia kwa kumwuliza:

**MWAVITA**: *"wewe ambaye hujaoa, utawezaje  kunieleza mimi juu ya kuishi na bwana? Unajua nini juu ya maisha hayo? Aisifuye……"*

Mama alimkatiza Mwavita. Hali halisi katika jamii ni kwamba mume na mke wanapotengana kupitia talaka, wote hukumbwa na changamoto tofautitofauti. Kwa mfano, wanawake wengi hawaruhusiwi kujumuika na kuzungumza na wanawake waliotengana na mabwana zao. Wengi hudhaniwa kuwa ni wachochezi. Kwa kifupi ni kwamba mke kama huyo huonwa na wengi kuwa mwasi na asiyefaa kujumuika wala kushauriana na wanawake wengine. Wanaume nao huonwa kama watu ambao hawana uwezo wa kumtunza mwanamke na wazururaji.

Walipokuwa wakielekea kutamatisha mazungumzo yao, mama aliwadokezea yale yaliyokuwa yakizungumzwa kule kijijini kuhusu Mwavita na Tenge. Kwamba, Mwavita ametengana na

Kinaya. Naye Tenge ana mimba ya pili. Mama alijaribu kudadisi kisha akagundua kuwa kuna kijana mmoja aliyejulikana kwa jina Kheri na mwenye tabia ya upole, ndiye aliyekuwa akiwatembelea. Mama alimkanya Tenge asirudie kosa la kupachikwa mimba mara ya pili.

Mwanamke aliyetengana na mumewe huchukuliwa kuwa mkaidi na asiye kuwa na maadili mema. Baadhi ya wanajamii humlaumu na kumchukia. Huonwa kwa mtazamo hasi. Horward (2011) katika kazi yake "*Nafasi ya dini katika ndoa tathmini ya Utengano* na *Paradiso*" anasema kuwa dini ni sehemu moja ya utamaduni wa watu, lakini dini ambazo zilikuja zina ubepari mwingi. Zilikuja na dhuluma za kisiasa na kijanja kutufanya sisi wajinga. Hasemi kwamba dini si muhimu, dini ina misingi ya kutufundisha kuwa watu bora, kutufundisha nidhamu…..Baadhi ya watafiti wametambua dini kama mojawapo ya asasi zinazowakandamiza wanawake. Kwa mfano, wakati ambapo Kinaya na mkewe walikuwa na mafarakano ya nyumbani, padre alijaribu kuingilia kati kwa sababu ya dini lakini juhudi zake hazikufaulu kuwaleta pamoja Mwavita na Kinaya. Hata hivyo tungependa kuunga mkono kauli kwamba, "dini yoyote ile ina dhima maalumu katika jamii-kuwafanya wanajamii wawe na maadili mema na kufuata kanuni pamoja na kaida zinazokubalika na wengi katika jamii hiyo".

## 2.5 NAFASI YA MAHAKAMA KATIKA SWALA LA NDOA NA UNYUMBA.

Mahakama ni sehemu ambayo watu wanaofikiri kuwa haki zao zimekiukwa, huenda kulalamika na kuzidai. Aidha ni sehemu inayotumiwa kutatua matatizo na mizozo ya kijamii kwa misingi ya sheria zilizowekwa. Uamuzi unaotolewa mahakamani ni wa kisheria ilhali unaotolewa vijijini na wazee ni wa kimaadili kupitia utamaduni.

Mwavita aliposhindwa kupata haki kutoka kwa wazee hakuwa na budi kuelekea mahakamani. Ijapokuwa alielekea mahakamani, hakufanikiwa kupata haki kamili aliyokuwa akitafuta.

Kinaya, Mwavita pamoja na jamaa wa kila pande walikwenda mahakamani ili kutafuta suluhu kutoka kwa hakimu kuhusiana na mzozo wao wa unyumba. Hakimu aliingia na kuanza kusikiliza kesi kuhusu talaka baina ya Kinaya na Mwavita iliyokuwa imeahirishwa. Mshitakiwa na mlalamishi walipofika mahakamani, kila mmoja alikuwa amejihami na wakili wake. Wakili wa kinaya hakuwa na mashahidi waliokuwa wamebaki kutoa ushuhuda wao. Wakili wa Mwavita aliieleza mahakama sababu alizopata kutoka kwa mlalamishi na mashahidi zilizomlazimu kuiomba mahakama itoe talaka.

Sababu ya kwanza ilikuwa ni kuteswa kwa kupigwa kulikosababisha kuavya kwa mimba na kung'oka kwa meno. Kwa hivyo ombi lake kwa wakili na mahakama lilikuwa ni, kumruhusu Mwavita atengane na mumewe kwa njia ya talaka. Wazazi kutengana si jambo geni, ni jambo ambalo limekithiri miongoni mwa jamii zote ulimwenguni. Ombi la pili ni mahakama kumweka mtoto Juma chini ya ulinzi wa mamake hadi atimie umri wa miaka kumi na sita. Ombi la tatu ni mahakama imwamuru mshitakiwa awe akimlipa mtaliki shilingi elfu moja kila mwezi za kumsaidia kumlea mtoto huyo. Maombi ya wanawake kupitia mahakama kuwaamrisha wanaume kutoa pesa kwa ajili ya malezi ya watoto wenye umri mdogo hadi miaka kumi na minane yameongezeka sana kwa sababu ya talaka nyingi. Ombi la nne ni mshitakiwa kuamrishwa na mahakama kumlipa mlalamishi gharama zote za kesi na ombi la mwisho Mwavita aliuliza mahakama itoe ilani kwa mshitakiwa asithubutu kwenda nyumbani kwa mlalamishi kwa kuwa kila mara aendapo huko huwa anazua rabsha na ghasia. (Uk. 99-100.)

Maombi haya yote yalipingwa vikali na wakili wa kinaya isipokuwa lile la talaka tu. Baada ya hakimu kusikiliza kutoka pande zote mbili, alitoa uamuzi. Uamuzi wa hakimu haukumfurahisha Mwavita na jamaa zake.

Hii ndiyo taswira ya baadhi ya mahakama zetu.Mwavita alitoa kauli kuwa hata sheria za nchi pia zinampinga. Mwavita alishuku kuwa hakimu alimpendelea Kinaya kwa sababu Kinaya na hakimu walikuwa marafiki wa siku nyingi waliokuwa wakistarehe ulevini pamoja. Hata hivyo mamake Mwavita alimtia moyo kwa kuwa:

> **MAMAKE MWAVITA:** *"Maadamu umepata kibali cha kujitenga na Kinaya umepata uhuru wako"*.

Baada ya kuona yaliyojiri, Tenge alitoa pendekezo kwa Mwavita kuwa wajaribu mbinu nyingine ili wapigane vita na kupata haki. Pendekezo lenyewe lilikuwa kujiunga na chama cha kina mama. Mwavita hakuona jinsi chama hicho kingewanufaisha. Tenge alifafanua kuwa chama cha kina mama kingeweza kuilazimisha bunge lichunguze sheria za jamaa na kuzifanyia marekebisho ili waweze kupata ulinzi bora. (Uk. 109.)

Pengine Tenge angetoa pendekezo la kukata rufaa kwenye mahakama ya juu maana kesi inapoamuliwa, hakimu huwa anatoa nafasi kwa mtu yeyote ambaye hakuridhishwa na uamuzi kukata rufaa.Hii inabainika kwamba walikuwa wameshindwa na mbinu iliyokuwa imebaki kwao ni kujiweka hadharani kwa umma aghalabu apate wa kumuhurumia. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi huchunguza miundo ya kijamii kama inavyofafanuliwa na mwandishi. Kwamba mawazo ya mwandishi alipokuwa akiandika hayawezi kulingana na mawazo ya msomaji anapokuwa akisoma. Kwa kifupi, madhumuni ya mwandishi na fasiri ya msomaji ni vipengele tofauti katika utanzu wa fasihi.

Hali kama hii iliyomkumba Mwavita ni yakini katika baadhi ya mahakama zetu kwa sababu ya ufisadi na mitazamo mbalimbali ya watu. Haki kamili kwa Mwavita pamoja na mtoto Juma haikutendeka kwa sababu kulingana na sheria ya watoto, mama anapotengana na baba, ni

muhimu mahakama kutathmini mienendo ya wazazi wanaotalakiana na kumweka mtoto upande wa mzazi ambaye atampatia haki yake na malezi mema. Sheria inatambua kuwa mtoto au watoto ni wa wazazi wote wawili ila wakati wa talaka, mtoto mwenye umri mdogo kama wa Juma angeweza kuachwa chini ya malezi ya baba tu; ikiwa maadili ya mama si mazuri, afya ya mama si nzuri na ikiwa mama si mtu anayejali masilahi ya mtoto. Uamuzi huu ulimfanya Mwavita kusema:

> **MWAVITA**: *"Najiona kama niliyegutuka ndotoni. Yale niliyoyadhania kuwa kweli sio kabisa. Nilipokuwa mdogo nilidhani kuolewa ni mbingu ya saba kwa mwanamke. Kumbe!" (uk. 90).*

Wakati wa dhiki hii ya Mwavita, Tenge alikuwa mtu wa karibu sana kwa kumpa mawaidha ya kumtuliza roho. Pia Tenge alikuwa na tajriba kuhusu mambo ya kimapenzi ndiposa akasema kuwa:

> **TENGE:** *"Zamani watu waliolewa, siku hizi watu wakutana wasukume masiku Kisha kila mtu afuate lake."*

Kulingana na tamthilia hii, baba alionekana kuwa na maadili mabaya na hakuwa mzazi aliyekuwa akijali familia yake kwa sababu ya uraibu wa ulevi. Ni yakini kuwa uamuzi kama huu lazima ungetiliwa mashaka.

## 2.6 UMOJA WA WANAWAKE.

Umoja wa wanawake ni swala ambalo kwa kweli limeangaziwa sana na makundi mbalimbali ya kijamii lakini linaonekana kupata pingamizi kali kutoka kwa wanamapokeo. Hata hivyo,

mikakati ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwafanya wanawake wafurahie uhuru wao imezaa matunda ijapokuwa bado kuna wanawake wengi ambao wamesalia katika hali ngumu ya maisha kwa sababu ya uoga na kutofahamu haki zao kisheria kama zinavyobainika katika sheria za nchi. Kwa mfano kuna sheria inayowaruhusu mke na mume kutengana lakini athari zinazoibuka kutokana na hali hiyo ya kutengana ni nyingi. Inawalazimu wakati mwingine waliotengana kutafakari kwa dhati kuhusu maisha ya watoto wao, kisha kuamua kurudiana bila masharti wala mpatanishi yeyote. Hali kama hii ilimpata Kinaya alipoamua kuzuru makazi ambayo mkewe alikuwa amehamia baada ya kutengana.

Tenge na Mwavita wakiwa ndani ya nyumba kwenye makazi waliyohamia baada ya kutengana, walisikia mungurumo wa gari likiingia na kusimama nje ya nyumba yao. Mtu akashuka na kubisha hodi. Bila kutarajia, Kinaya aliingia akiwa mlevi. Jambo hili lilimfanya Mwavita kushtuka. Kinaya akajaribu kumrai Mwavita warudiane lakini mara tu alipotaja jina la mwanawe Juma, hasira ilimpanda Mwavita, akamwuliza Kinaya kuondoka kwa utaratibu. Kukawia kwa kinaya kulizua ugomvi na kisha vita baadaye. Katika harakati za vita , Kinaya alizidiwa nguvu na kina dada hawa wawili. Walishirikiana kumchapa hata ingawa Tenge alijaribu kuonyesha huruma na mwishowe wakamvua longi na shati akabaki na chupi kisha wakamrusha nje na kumtaka apeleke malalamiko kwenye kituo cha polisi. Baada ya Kinaya kuondoka, kina dada hao walianza kutathmini jinsi kuungana kwao kuliwanufaisha kwa kumpa Kinaya funzo maalumu. Kisa cha vita hivi kilimkumbusha Tenge ngonjera ya 'umoja wa kina mama'. Ngonjera hii inapatikana katika utangulizi wa tamthilia ya *Mama Ee* Kukosa umoja miongoni mwa kina mama ndiko huwafanya kupitia hali ngumu ya maisha. Walipomaliza kutathmini jinsi walivyofaulu kumwadhibu Kinaya, waliamua kwenda kwenye ofisi ya chama cha kina mama.

Walipofika pale waligundua kuwa ofisi yenyewe ilikuwa imepambwa vizuri sana. Wote wawili wakakubaliana kwamba chama kipo lakini umoja wa kina mama haupo.

Kuna tabaka la kina mama wasomi ambalo idadi ya wanachama wake wengi hupatikana mijini. Idadi yao si kubwa ikilinganishwa na tabaka la wanawake walioko vijijini. Wanawake walioko vijijini ni wengi kiasi kwamba wakiungana na idadi ndogo iliyoko mijini matokeo yatakuwa ya mafanikio. Watakuwa na hakika ya kufaulu kupigania na kupata haki zao.

## 2.7 KIMALIZIO

Katika tamthilia ya Mama Ee, msanii amedhamiria kutuonyesha jinsi baadhi ya jamii zetu na baadhi ya familia zinavyoishi katika hali ngumu. Kwamba mali haiwezi ikamletea mtu furaha maishani bila kuwa na amani katika maisha. Kila tabaka lina changamoto za kipekee na changamoto hizi husababishwa na binadamu yule yule ambaye yuatafuta raha bila kujali athari za wale wanaomzunguka. Kinaya na kakake Tenge ni mfano wa kundi hili. Kinaya alikuwa mlevi sugu na alisahau kuwa kabla hajapata kazi, wazazi wake walihangaika na kumtunza, yeye hana habari kumhusu mwanawe Juma. Ndiyo maana anamwachia mkewe akihangaika naye bila sababu maalumu ya kutoshirikiana wote wawili. Katika kazi hii tuligundua kwamba utamaduni, mila na desturi hutumiwa na baadhi ya wanajamii kujinufaisha na kuwapora wasiofuata mila. Mfano mzuri tunaoweza kutoa ni yale malipo Kinaya alitozwa na wazee. Wanaofaidi ni wengine, si Mwavita aliyepigwa, akadhulumiwa na kujeruhiwa.

Msanii alidhamiria kutuonyesha kuwa, mwanamke akiamua , ana uwezo wa kupigana zaidi kuliko mwanaume. Kinaya alipozidi, Mwavita aliamua kukabiliana naye bila kujali mila na desturi. Alimkabili Kinaya kama simba na kumvua nguo zote isipokuwa ile ya ndani tu. Tabia ya ulevi kupindukia humwathiri mhusika kwa kumpunguza nguvu za kiutendaji katika nyanja zote

za maisha na kubadili mwenendo wa muhusika. Kwa mfano ulevi ulimfanya Kinaya aipuuze familia yake, akawa analala kwenye vilabu, akakosa heshima kwa mkewe na wakweze na mawazo yake yakakosa mantiki kulingana na mienendo pamoja na matarajio ya jamii kwa mtu mwenye hadhi na msomi kama yeye.

Wakati mwingine, si rahisi wanawake kuwa na muungano ili kutetea haki zao ila inapowalazimu. Mwavita alikiri kuwa chama cha wanawake kilikuwepo lakini muungano wa wanawake haukuwepo. Walidhamiria kuwaunganisha wanawake wa matabaka yote. Jambo lililowashangaza ni kule walipoingia kwenye ofisi ya chama cha muungano wa kina mama na kumkuta mama mnene ambaye ndiye alikuwa kiongozi wa kikundi hicho. Walipojaribu kumweleza kiini chao cha kuizuru ile ofisi, aliwaambia kuwa chama chao hakikuundwa na kupatiwa majukumu ya kusuluhisha matatizo yanayozikumba familia; kisha akawauliza waharakishe kwa sababu mumewe alikuwa karibu kumfuata na kumchukua nyumbani kwa gari.

Kina dada hao wakiwa pale ofisini, waliona jinsi ambavyo wanawake wengine walivyokuwa wakiletwa na bwana zao kwa magari ya kifahari. Bila shaka uzoefu huu lazima ulimkumbusha Mwavita kuwa mumewe waliyetalakiana alikuwa na gari lakini hakufurahia maisha ya kuwa na gari walipokuwa wakiishi pamoja. Kuna baadhi ya watu walio na magari ya kifahari, lakini ajabu ni kwamba badala ya mali hiyo kuleta raha maishani mwao, inaleta karaha.

Baada ya kufanya uchambuzi na uchanganuzi wa tamthilia ya *Mama Ee* kwa kina tumegundua kuwa jamii huwa na matarajio mbalimbali kutoka kwa mwanamke. Matarajio hayo ndiyo yamechangia wanafasihi kumchora mwanamke katika kazi zao kwa njia mbalimbali kama inavyobainishwa hapa chini. Mwanamke amechorwa kama mtu ambaye maisha yake siku zote yamo mashakani na mwenye kulalamika kila mara. Haijalishi yumo kwenye tabaka gani. Katika

utangulizi wa tamthilia ya *Mama Ee*, wanawake wale watatu na ngonjera yao wanatuthibitishia kauli hii. Mwanamke amechorwa kama kitega uchumi, wakati msichana anapochumbiwa ili apate kuolewa baadhi ya jamii nyingi huitisha mahari kama vile ng'ombe, mbuzi au fedha kiwango fulani. Wakati ugomvi unapozuka si ajabu kumpata mwanaume akimfukuza mkewe na kudai mahari aliyotoa kabla au baada ya kuoana. Hata hivyo vijana wa karne ya Ishirini na moja wana mtazamo tofauti kuhusu maisha yao ya unyumba na swala la mahari. Kulingana nao, kinachopewa kipaombele ni maisha ya kifantasia. Kuna wachache ambao wanashikilia mtazamo kuwa wasichana wanauzwa. Katika tamthilia hii tunawapata baba mkubwa wa Mwavita pamoja na Kinaya mwenyewe wakithibitisha kauli hii pale Kinaya aliposema kuwa babu zao hawakulazimishwa kulipa pesa zaidi ati kwa kuwa mke ana shahada! Lakini wazazi wa siku hizi wanawauza mabinti zao. Naye baba mkubwa Mwavita akasema kuwa zamani wao walioa wake lakini sasa watu wananunua…..

Mwanamke amechorwa na kufananishwa na ngoma. Kwa kawaida ngoma ni ala ya muziki ambayo hupigwa na kutoa sauti yenye ridhimu (mapigo/mdundo). Sasa wanawake ingawa si wote ni ngoma ya kupigwa na kusikilizwa wakati wanapotoa mlio au wakati wanapopiga nduru. Mwanamke ana taswira ya mtumwa. Mtumwa ni mtu ambaye hana uhuru. Ni mtu anayeamrishwa kutekeleza majukumu bila hiari yake mwenyewe. Mwavita alidhibitsha kauli hii katika aliposema kuwa, mke mtumwa tena ua la kujigamba shereheni-mtumwa kimwili-kiakili kiroho-kila kitu.Mke hajui kuwa yeye ni mtumwa!

Jinsi ambavyo Mwavita alipokuwa akiamrishwa na kulazimishwa na mumewe kuamka na kumpikia usiku wa manane ni dhihirisho kamili la kauli hii. Mwanamke aliyeolewa anachukuliwa kama mtu ambaye hawezi kumiliki chochote (hii ni katika baadhi ya jamii kama

hii ya Kinaya). Kauli hii tunaithibitisha kwa kurejelea usemi wa Kinaya kuwa: Mwanamke hana chake. Akishaolewa kila kitu hata yeye mwenyewe ni mali ya bwana wake.

Mwanamke ni mpishi wa mumewe. Mtazamo huu ulionekana kwa nyanyake Mwavita alipomuuliza Mwavita sababu iliyosababisha akaamua kumnyima mumewe chakula ilhali hili ni jukumu la mwanamke hata kama mumewe ni mlevi kiasi gani. Ni lazima ampikie yeye na wanawe.

Ingawa tamthilia *Nimelogwa nisiwe na mpenzi* ya Ngugi G. (2011) si miongoni mwa zile tulitumia katika uchunguzi wetu kuhusu 'taswira ya mwanamke…,' katika tamthilia hiyo ametuonyesha taswira ya mwanamke kupitia wahusika wake Mathew, Jane, Beatrice na Ronald. Tamthilia hii ina matukio ambayo yana ukuruba mwingi na *Nguzo Mama* na *Mama Ee*. Tunampata Ben ambaye ni kijana msomi lakini hajaoa kwa sababu amekuwa akiendelea na masomo ilhali vijana wa rika lake wameshaoa karibu wote kijijini mwao. Kuna binti mmoja wa rafiki ya babake ambaye anapendwa na Ben sana lakini yeye hampendi Ben. Huyo binti anajulikana kwa jina Beatrice. Ben alidhani kuwa huyo binti hakumpenda kwa sababu ya mavazi. Ndipo tunamwona Ben akitafuta njia ya kumlaghai rafiki yake Mathew kuwa ana safari ya kwenda Nandi kwenye sherehe ya rafiki yake na anamsihi Mathew amuazime nguo, kofia na viatu. Mathew alipogundua kuwa Ben alimlaghai, alikula mori akaanza kumsaka Ben. Alipomkuta Ben wakiwa na Beatrice, Mathew alimshambulia na kumdunga kwa kisu Ben mara kadhaa mbele ya Beatrice na kumwacha hoi. Badala ya Beatrice kuhuzunika na kuogopa alimpongeza Mathew.

Mathew na Beatrice waliendelea na mazungumzo yao ambayo yaliashiria kuwa Mathew alikuwa na mpango wa kumwacha mkewe Jane na kutengana naye kabisa ndiposa tunampata Mathew

akimweleza Beatrice kuwa: aliyotukia ni kwa sababu walikuwa wanajifurahisha tu bila matumaini maovu lakini kwa bahati mbaya maafa yakawaingilia, naye Jane akapata mtoto. Hata hapakuwa na harusi ya haja kwani hata mlango wa kanisa hawakuufikia. Alimnunua tu kama vile angalivyo mnunua mbuzi sokoni.

Mathew sasa hamtaki Jane. Wamlipe wasimlipe yeye angali kijana atapata mwingine. Aliendelea kumweleza Beatrice kuwa: tangu Jane alipopata mtoto, amekuwa mchafu tena mvivu, hata kushonea nguo kifungo anaona shida sana.

Usemi huu wa Mathew unadhihirisha jinsi baadhi ya wanaume ambao wameingia katika maisha ya unyumba mapema wanavyowaza na kujidanganya baada ya kutimiziwa haja zao. Wengi ambao wamekuwa na mawazo kama haya wameishia kutangatanga kisha kufa bila kuwa na familia inayoeleweka katika jamii. Mahaba yalinoga na walipokuwa wakiendelea na shughuli zao, Jane akawafumania wakipigana busu. Wakati Jane alipomwuliza mumewe kuhusu kitendo cha kumdunga Ben kisu, Jane aliamrishwa na Mathew kunyamaza ama afanywe jinsi Ben alivyofanywa. Mathew aliendelea kumwambia kuwa ailimnunua tu kama mbuzi na sasa amemchosha. Na kwa sababu hawezi kumchinja akamla atamtupilia mbali!

Ushahidi huu unathibitisha baadhi ya dhuluma ambazo Katola (2006) alitaja kuwa wahusika wa kike wanadhulumiwa kwa njia ya matusi. Kwa mfano, Beatrice alimkabili Jane kwa kumwambia anyamaze kwa kuwa yeye ni mbuzi. Jane naye kwa hasira akamwambia Beatrice kuwa hawezi kunyamaza kwa kuwa Beatrice ni dude tu tena kirukanjia wa mtaa mzima asiye na adabu.

Kulingana na Ngugi, au kupitia kwa kazi yake hii, tumegundua kuwa mwanamke amechorwa kama kitu cha kununuliwa na kuuzwa. Kwa muktadha huu, ni kiumbe kwa jina mwanamke au

msichana ambaye anaweza kuamrishwa, kutumiwa wakati mume anapotaka kujifurahisha na kisha kutupwa.

Kama kazi hii inavyodhihirisha, ni yakini kuwa hatua yoyote ambayo mtu ameamua kuchukuwa ni lazima iwe na manufaa au hasara kwa mtu binafsi, familia na jamii. Sheria, mila na desturi zinaruhusu kila jamii ifanye juhudi kuhakikisha ya kwamba miundo msingi ya kijamii ni thabiti ili kuleta mshikamano wa familia na taifa. Mshikamano wa kitaifa ni muhimu na iwapo familia haziwezi kuhakikishiwa usalama, ukuaji na maendeleo vitasambaratika. Ukosefu wa usalama nyumbani utazifanya familia nyingi kutengana na Njagi katika jarida lake kuhusu familia, anafafanua kuwa familia zilizo na mzazi mmoja ni zile ambazo mzazi huyo huchukuwa majukumu ya kuwakuza watoto peke yake. Kuna aina mbili za familia zenye mzazi mmoja-zile ambazo kwa wakati fulani zilikuwa na wanandoa na zile ambazo mtu hajawahi kushiriki ndoa tangu kuzaliwa. Familia za mzazi mmoja huweza kusababishwa na mambo mengi yakiwemo talaka, kifo, kutengana, kifungo cha maisha, ugonjwa na kususia familia. Katika nchi ya Kenya sababu hizi zote ni halisi kwa watu tofautitofauti. Kulingana na tathmini ya Njagi, familia zilizo na mzazi mmoja zina idadi nyingi ya wanawake ambao ni wajane, waliopewa talaka au waliotengana. Anatamatisha kwa kusema kuwa, mzazi akiwa peke yake hukumbana na changamoto nyingi kama vile jukumu la kuwalea watoto peke yake, upungufu wa fedha za kuyakimu mahitaji, kuwapa watoto ambao wameanza kubalehe nidhamu, usumbufu kutoka kwa mashemeji, upweke, kutuhumiwa na watu juu ya suala la maadili, baadhi ya jamii kumlazimisha mjane arithiwe, watoto kukua wakimfahamu mzazi mmoja na upungufu wa mawasiliano baina ya watoto (hasa vijana wa kiume) kadri wanavyozidi kukua. Maswala yote yanayowakabili wanawake ni nyeti na yasipoangaziwa kwa jicho pevu yataleta athari mbaya kwa familia, jamii na nchi.

# SURA YA TATU

# UCHAMBUZI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA YA *NGUZO MAMA*

## 3.0 UTANGULIZI

Tamthilia ya *Nguzo Mama* ni kazi ya sanaa ya fasihi ambayo imeandikwa na Penina Muhando kwa ustadi mwingi na inamulika changamoto zinazomkumba mwanamke katika baadhi ya jamii zetu. Kwa sababu binadamu ni kiumbe wa kufikiri na kutenda, mikakati imewekwa na kina mama ili waweze kukabiliana na changamoto hizo. Wajibu wetu kwenye kazi hii ni kuchambua na kuchanganua tamthilia hii ili kuyafikia malengo yetu ya utafiti. Kurunzi yetu kwenye kazi hii ni nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Kwa mujibu wa Mbuthia (2005), juhudi kubwa zimefanywa ili kupata uelewa wa ndani kuhusu jamii kupitia uchunguzi wa kina wa kazi iliyoandikwa. Hii itawezekana tu, ikiwa mtafiti atateua nadharia inayofaa. Kazi za Wellek na Warren (1978) zinabainisha wazi uzuri wa Sosholojia ya Fasihi. Kwa kazi hii tunayoifanya (taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee*), nadharia hii imetufaa.

Uchunguzi wetu pia unakubaliana na mtazamo wa Zhadnov, kwamba kazi ya sanaa hutupa mwonekano halisi wa jamii. Kazi hii ya Muhando ni miongoni mwa kazi ambazo zimechapishwa ili kuonyesha juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa tangu mwaka wa 1975 kuwakomboa wanawake kutoka ukandamizwaji na udhalilishwaji kupitia asasi mbalimbali za kijamii kama vile ndoa na utamaduni. Kazi zingine ambazo zimechapishwa zikiwa na madhumuni yaya haya ni *Pango*, *Natala*,riwaya ya *Nguvu ya Sala*, *Wingu Jeusi* na *Kilio Cha Haki*.

### 3.1 SWALA LA UTABAKA NA WANAWAKE

Utabaka ni istilahi inayotumiwa kurejelea kundi la watu, mimea au wanyama kwa misingi inayobainika na kuonyesha utofauti au ubaguzi. Swala la utabaka limekita mizizi miongoni mwa jamii nyingi za kibinadamu. Ni swala la kiasili katika maisha ya kibinadamu japo wakati huu limeonekana kuwa changamoto kwa sababu ya itikadi na mitazamo ya watu kulingana na hadhi zao. Katika hali ya kawaida ni bayana kuwa watu wakikutana sehemu fulani kwa mfano kwenye hafla ya harusi au maziko, utabaka utajitokeza. Utabaka unajitokeza kwa sababu ya mitazamo ya watu na ubinafsi. Kila mtu ana ubinafsi unaomtambulisha kama "yeye". Ubinafsi huu hutokea kulingana na akipendacho au akichukiacho mtu. Hisia za mapenzi au chuki haziwezi kudhibitiwa hivi hivi kwa urahisi. Ndio maana kwa kuegemea dhana hii, watu aidha wa jinsia moja au tofauti wakiwekwa pamoja, wataanza kujitenga kivikundi na huo ndio mwanzo wa utabaka na ubaguzi. Kauli hii inadhibitishwa na Coser (1963) kama alivyomnukuu Honore de Balzac (1799-1850) na kueleza kuwa:

> "Ukiwa na familia ambazo hazina uwezo unaolingana kimaisha katika sehemu yoyote ile, utaona utabaka ukijitokeza"

Nadharia yetu inatusaidia kuchunguza masuala kama haya jinsi yanavyoiathiri mifumo mbambali ya kijamii ambayo ndio chanzo cha kuwepo fasihi. Hali ya utabaka ilijitokeza kabla igizo kuanza kwenye jukwaa. Kibwagizo cha wimbo kilisikika ndiposa mwanamke ajulikanaye kama BI MOJA aliyekuwa amevalia Kimwambao akatokezea na kuelekea kwenye sanamu iliyokuwa na kibandiko chenye maandishi "NGUZO MAMA." Kibandiko hiki ni taashira ya kuleta umoja wa wanawake. Matamshi ya BI MOJA yalitupatia picha kuhusu mawazo yake, tabaka na mazingira alimotoka. Kisha BI PILI aliingia na maelezo tuliyopata kumhusu, ni

mkulima aliyekuwa mwenyeji wa bara. Kulingana na usemi wake, ilidhihirika kuwa ni mwanamke aliyetoka kijijini mahali ambapo mfumo wa familia ulionekana kuwa wa wanachama wengi ambao wanajumuisha jamaa wa karibu kama vile shangazi na mjomba. Hatimaye BI TATU aliingia huku akiwa amevaa vitenge vya Kizaire. Huyu alionekana mwenye uwezo tena wa tabaka la juu kwani mapambo aliyopendekeza wayatumie kupamba NGUZO MAMA ni ya thamani kama vile mabenzi na mavolvo (aina ya magari ya kifahari). Mabibi hao wote walishirikiana ijapokuwa ni kwa mda mfupi, wakajaribu kuiinua ile NGUZO MAMA lakini haikuinuka kutoka pale wala kuonyesha dalili ya kusonga hata inchi moja. Ndiposa msimulizi akaanza hadithi na akatupeleka hadi mandhari ya vijijini hasa kwenye kijiji kilichojulikana Patata. Patata ni kijiji ambacho kilikuwa kimesifika sana lakini wahenga walisema, "Uzuri wa nyumba si mlango, hebu fungua uingie mle ndani." Msimulizi alianza kwa kusema kuwa:

**MSIMULIZI**: *"Kwa wa nje iling'ara*

*Kwa vicheko vya wake wana*

*Vilema vyao walivijua*

*Vurugu na matata Patata vikajikita*

*Maendeleo yakawa hatarini*

*Kwani wabeba wana vibaya walinyanyasika*

*Wakaonekana si watu*

*Ingawa jamii waliikuza."( UK.5.)*

Maelezo haya ya msimulizi yanatupatia picha kamili jinsi wanawake wanavyopitia masaibu kwa kunyanyaswa na kulemazwa. Ilibidi la mgambo kulia ili kina mama wapewe NGUZO (uhuru na uwezo) kwa sababu, "la mgambo likilia,lina jambo!" Watu wote walikuwa na ari ya kutaka kufahamu dhana ngeni hii ya NGUZO MAMA, ndiposa kina baba wakagundua kuwa wamo hatarini. Ni kweli kwamba, Msimulizi anatueleza kuwa:

> **MSIMULIZI:** *"Moyoni walijiwazia wengine wazi walijisemea. Imeandikwa NGUZO MAMA. Hiyo NGUZO MAMA yao hao wabeba wana, waachieni wenyewe mambo wajitengenezee. Kwani maendeleo ya Patata si ya wake na waume?" (uk.8)*

Usemi huu unadhihirisha aina tofauti ya mifumo ya kijamii ambayo tunayo na jinsi baadhi ya wanajamii wanavyokuwa na mitazamo tofautitofauti kuhusu wazo lolote ambalo limeibuka kutoka kwa tabaka la jinsia ya kike. Mmoja wa wazee kajiamulia kuwa akirudi nyumbani, atamwambia mkewe: "*mama wa wanangu 'pole!*."

Wabeba wana walijaribu kuisimamisha Nguzu Mama bila kufanikiwa. Ndiposa wakaamua kuitafuta siri (kiini kinachosababisha Nguzo Mama isisimamishwe). BI NNE aliingia huku amevalia vitenge na kilemba. Akatoa mapendekezo kuwa ili waweze kuupata uhuru wao,ni lazima wafanye mikutano, maandamano na kutoa maazimio. BI TANO na BI SITA waliingia kwa miondoko yao. BI TANO kwa miondoko ya ngoma ya Madogori na BI SITA kwa miondoko ya kikahaba huku akiwa amevalia kikahaba. BI SITA anatudokezea muda ambao amekuwa mjini na jinsi amefanya kazi yake mjini kwa kusema kuwa:

> **BISITA:** *"Mji huu sikuingia leo ndugu yangu. Mawaziri, makabwela, mapadre kwa mashehe, vijana kwa wazee mie breki mie jeki."*

Hii ndiyo taswira ya makahaba. Hawachagui wateja, kila mtu kwa zamu yake mradi tu ana hela za kulipia huduma. Maswala kama haya hatungeyafahamu kwa sababu si rahisi kukutana na muhusika huyu ana kwa ana akatusimulia, lakini kwa sababu ya usomaji wa kazi za sanaa inayotumia lugha tunawezeshwa kuyachunguza na kuyatathmini maandishi haya ya fasihi ili kuelewa ni athari gani maudhui ya kazi hii yataleta katika jamii.

BI SABA naye akaingia na kuondoka bila kusema chochote wala kujaribu kuinua NGUZO MAMA. Yeye ni kiwakilishi cha mwanamke aliyepitia maisha magumu na kuchanganyikiwa hata ingawa kimya kina kishindo. Kisha msichana mwenye umri mdogo ambaye alikuwa amevaa sare akaingia jukwaani. Sauti mbalimbali zikamwita: "njoo huku" kabla hajaenda, "njoo huku" mpaka akachanganyikiwa kwenye mtanziko huo, akashindwa aende wapi. Hii ni taswira ya jinsi mtoto wa kike anapatiwa majukumu mengi kwenye baadhi ya jamii na familia vijijini na mijini. Watoto wa kike hupewa majukumu mengi kama vile kusomba maji, kufagia nyumba, kusafisha vyombo, kukusanya kuni, kupika, kuchuma mboga, kusaga, kulea watoto na kwenda shuleni. Kwa sababu ya majukumu mengi wanayotwikwa watoto wa kike, maendeleo ya kimasomo huathiriwa hasa wakati wa mitihani ya kitaifa. Changamoto zinazowakumba watoto wa jinsia ya kike ni nyingi.

BI NANE alikuwa mtu wa mwisho kuingia. Alionekana kuwa msomi tena mwenye hadhi ya juu. Yeye hakusema chochote ila alitafakari, akaimba kama wengine walivyofanya kisha akatoka. Mikutano ya kina mama kwa ajili ya kupigania haki zao imekuwa ikifanyika tangu mwaka wa 1975 hadi leo hii ila imekuwa ikikabiliwa na changamoto ambazo zimejitokeza kwenye tamthilia hii. Kukosa muungano na umoja wa kina mama ndicho kizingiti nyeti ambacho kimezuia uhuru kamili wa wanawake usipatikane.

## 3.2 TAASHIRA YA UMOJA

Taashira ni ishara au alama maalumu zitumikazo katika jamii kuwakilisha tendo fulani katika jamii hiyo. Musimlizi anashangaa ni vipi Nguzo Mama itatolewa bure halafu ikose kusimamishwa. BI NANE alitoa mapendekezo na ushauri kuwa, ili Nguzo Mama iweze kusimamishwa, lazima waivute kwa kamba pamoja. Kamba hapa iliashiria umoja na muungano wa wanawake ili kupata uhuru wao ambao umetolewa bure kupitia azimio la umoja wa mataifa. Wazo la BI NANE lilipingwa vikali sana na BI NNE aliyekuwa na fikra kwamba mamlaka yake yamo hatarini. BI NNE alihoji:

> **BI NNE** *"alikuwa wapi wakati NGUZO MAMA ilitolewa na wala hakuonekana kwenye harakati za maandamano?"*

Msimulizi alitabiri kuwa, hali ikiendelea jinsi ilivyokuwa, zogo litatokea kwa sababu kila mtu afanya lake akiamini lile afanyalo. (UK.17.) BI PILI aliamua kujipikia pombe na kuiuza kilabuni ili apate pesa za kujikimu maishani. Yeye alidhani kuwa Nguzo Mama haikusimama kwa sababu hakuwa na pesa. Dhana hii ina uzito fulani kwa sababu hata Woolf (1929) alidai kuwa:

> "mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajajikomboa kiuchumi".

Mtazamo huu wa Woolf ni kama wa Beauvoir (1949) anayeamini kuwa, ili mwanamke kupata ukombozi kamili ni lazima awe ameimarika kiuchumi. Kwa bahati mbaya, BI PILI alidhamiria kuwauzia pombe hiyo wanaume walio na wake kama yeye. Tuligundua kwamba, ulevi ni chanzo cha ugomvi, vita na mafarakano kwenye baadhi ya ndoa kama vile ya Mwavita na Kinaya katika tamthilia ya *Mama Ee*. BI PILI alibahatika kuwapata wateja ambao ni Totolo na Shaba. Totolo na Shaba walidhani kuwa Nguzo Mama ni dhana ambayo wanawake walizindua kuteleka na kuwauzia pombe ili wainue uchumi wa Patata. Baada ya kuonja Totolo na Shaba

waligundua kuwa kile kinywaji kilikuwa kitamu zaidi. (UK.18.) BI PILI alishangilia kuwa kinywaji chake kilipata wateja. Ghafla bin vuu mumewe Sudi aliingia amelewa chakari akazua fujo na kumwitisha mkewe pesa alizokuwa amepata kutokana na mauzo yake ya pombe. Kulewa kwa Sudi kulitokana na pombe ya bure aliyokuwa amekunywa nyumbani kwake kisha akaenda kunywa nyingine huko nje. Alimlazimisha mkewe ampatie pesa aende kununua pombe kwingine. Mkewe alijaribu kujitetea kwamba hakuwa amepata hela na pia hata kama angekuwa amepata, kuna matatizo chungu nzima nyumbani yaliyohitajika kutatuliwa na hizo hela alizokuwa akiuza pombe. Sudi akamwambia:

> **SUDI**: *"Wacha mdomo, nitakupiga mbele ya hawara zako."(Totolo na Shaba). (UK.19.)*

Hatima ya majibizano baina ya Sudi na mkewe ni vita ambapo tunaona BI PILI alipigwa na kutoroka. BI MSIMULIZI anaeleza kuwa:

> **MSIMULIZI:** *"Upishi wa pombe balaa ulimzushia visa na mikasa BI PILI. Pesa alizipata kutokana na mauzo ya hiyo pombe. Lakini visa vya pombe hiyo pesa hazikufidia. (UK.20.) Pombe zikatapakaa kila mahali. Patata ikatingishika pombe kushika hatamu. Kazi kando ikawekwa ikabaki ya kunywa pombe. Pesa zikapatikana. Hizo hizo pombe zikanunua. Na ile NGUZO MAMA udongoni ikabakia"*.

Pombe ni kinywaji kinachochukuliwa kuwa cha maana miongoni mwa jamii nyingi nchini Kenya, lakini madhara yake yamekuwa mengi. Kinywaji hicho hutumiwa na baadhi ya jamii wakati wa sherehe maalumu kama vile harusi, tohara, matambiko, kupatanisha jamaa waliokosana na baada ya maziko. Zamani pombe ilidhibitiwa kupitia kanuni zilizowekwa lakini siku hizi juhudi za viongozi za kukabiliana na tatizo hili zimekumbwa na changamoto nyingi.

Kwa sababu hii pombe imesababisha madhara mengi kama vile wanawake kupigwa na kuuawa, talaka, ajali barabarani, wizi wa vyombo vya nyumbani na kukosa kuwaelimisha watoto.

Humu nchini mwetu biashara ya kuuza pombe haramu imekithiri katika miji mikuu. Pale vijijini hali ni hiyo hiyo kwa sababu ya kiwango cha umaskini ambao umekuwa wa kiwango cha juu.

BI MOJA alikuja na wazo geni tena nzuri la kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mapambo ya nyumbani ili yauzwe na kuinua hali yao ya uchumi. Biashara hii ilianzishwa kwa ushirikiano na umoja ikashika moto na mauzo yakawatia moyo na matumaini lakini kadri muda ulipozidi kuyoyoma, soko lilikosa kwa sababu karibu kila mtu alikuwa amenunua vitambaa vya kutosha. Kikundi kilianza kusambaratika wakati BI TANO alipokosa soko la kuuza na kurudi na mali yote. Chizi alimtathmini BI NANE ifuatavyo:

**CHIZI***: "Huyu Bi Nane mimi*

*Naogopa kumsogelea*

*Nisije kuambiwa "My god".*

*Sana wanamchukia*

*Hasa huyo Bi Nane*

*Lakini sana nikimsikiza*

*Ingawa mimi "my god"*

*Maneno yake ni kweli*

*Lakini nao wenzake*

*Kumsikiza hawataki*

*Nimeshindwa sababu kuielewa”. (uk.70)*

BI NANE alikuwa ametoa wazo la kutumia kamba kuinua NGUZO MAMA lakini kwa sababu ya chuki na utabaka, BI NNE alimshambulia vikali sana. Kamba hii iliyopendekezwa kutumika iliashiria umoja na ushirikiano wa wahusika wote.

Kuna aina ya watu ambao hawafi moyo kwa sababu ya kupata upinzani mkali. BI NANE ni miongoni mwa kundi hili. Licha ya upinzani mkali na kukosolewa, alidhamiria kuwaalika wanaume na vijana kushirikiana kuisimamisha ile NGUZO MAMA.

Baada ya lile kundi la kwanza kusambaratika, BI NANE alianzisha kikundi kingine kilichodhamiria kuwafunza vijana wapate mafunzo ambayo yangewawezesha kuwa na maarifa ya kuisimamisha ile Nguzo Mama. BI NNE alipogundua kuwa BI NANE ameanzisha kikundi kingine, aliaalika kikao cha dharura. Lengo la kikao kile lilikuwa kuwazuia BI NANE wasiendelee na mipango yao ndiposa mwenye kiti wa kina mama akasema:

> **MWENYEKITI:** *“Tumepata habari kwamba wewe umeanzisha kikundi cha kupinga juhudi za wenzetu hapa Patata za kusimamisha NGUZO MAMA. Tena kikundi hichi cha walimu watupu kinabagua wasio walimu. Kikundi hicho kimekuwa kikipanga njama za kuchafua juhudi za wenzenu.”*

BI NANE alionekana mtu mwenye hekima na busara. Hakuyaendea mambo kwa pupa. Baada ya kutafakari na kutathimini alijisemea kimoyomoyo:

> **BI NANE**: *“jihadhari mwanakwetu makubwa sijizulie. Kofia za kiongozi wenzio*

*wamezivaa. Nijuavyo mie, kofia mengi zafunika mvi, makovu, vipara, mawazo ya kila aina, maovu na mema."*

BI NANE aliamua kunyamaza bila kujibu wala kuuliza. Kimya kingi kina kishindo, tena ni silaha kali. Kimya huashiria kutafakari, dharau au hasira. Baadhi ya watu hunyamaza wanapokasirishwa na jambo fulani, swali au kauli ya mtu.

Kwenye kikao hiki cha dharura BI NANE aligundua kuwa baadhi ya washirika wake hawakuwa waaminifu. Walikuwa na tabia ya kuchukua taarifa na kumpelekea BI NNE. Hali hii ni yakini miongoni mwa wanajamii inatukumbusha yale Mwavita alimwambia mamaye kuwa:

**MWAVITA:** "*adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake, si mwanaume pekee."*

Wakati mwingine ni vigumu sana wanawake walio na utabaka na hisia tofauti kujumuika na kufuatilia lengo au malengo maalum ya kikundi. Baadhi ya mawazo yanayotolewa na wale walio na uwezo huwa yanapokelewa kwa mtazamo hasi na wale ambao hawana uwezo hasa kiuchumi. Kuna mashindano fulani baina ya matabaka haya mawili. Kinachopungua hapa ni elimu na maarifa au ufahamu. Ndio maana tunakubaliana na maoni ya Wollstone Craft (1972) kuwa, elimu ndiyo msingi wa kila kitu maishani na kukosa elimu ni kukosa kitu chenye thamani maishani.

Hasira zilimpanda BI NANE lakini vyema akazitawala. Aliweza kung'amua kuwa kikao kile kilikuwa cha hila kwa sababu hakuna katiba inayoruhusu watu wawili wafanye kikao bila wanachama wengine kuwepo au kutuma udhuru, akaendelea kunyamaza. Baada ya mwenyekiti kutoa ushauri, BI NANE aliamua kuvunja kimya chake. Tunamwona akikataa katakata kuwa hatachukua ushauri wowote kutoka kwake. BI NNE alijaribu kuchochea, lakini mshitakiwa akamwomba mwenyekiti ailinde haki yake ya kuzungumza. BI NANE akaeleza kuwa hawezi

kupokea ushauri kwa sababu hajasikia shitaka lake likisomwa. BI NNE alimshambulia BI NANE kwa sababu ya uhasama uliokuwepo baina yao kwa kusema kuwa:

**BI NNE:** *"Hayo madigirii wanayoringia anataka kuyaleta hapa. Na hilo ndilo tatizo. Hawa walimu hasa huyu BI NANE wanaringa sana na madigrii. Hawajui kwamba hao hao wanaowadharau ndio waliowasomesha mpaka kuyapata hayo madigrii."*

BI NANE alimsihi mwenyekiti amruhusu ajieleze kwa njia ya maandishi, BI NNE akapinga wazo hilo na kumwambia BI NANE kuwa:

**BI NNE:** *"mwenyekiti huwa yuko tayari kujitetea siyo mpaka aandike. Siyo kutuletea tabia za kisomi hapa."*

Mvutano ulioibuka kati ya BI NANE na BI NNE, ni kielelezo ambacho kinatufungua macho na kuelewa sababu ambazo zinawafanya wanawake wakose umoja na ushirikiano-wivu, mashaka, fitina, chuki, faraka, uzushi,ubaguzi na madharau ni vizingiti vikuu vinavyosababisha umoja wa kina mama kuwa adimu.

### 3.3 WANAWAKE NA WATOTO WA KAMBO

Watoto wa kambo ni istilahi inayotumiwa kuwarejelea watoto ambao wamezaliwa kwa mama mmoja na kulelewa na mke mwenza. Ni tabaka la watoto wanaokumbana na matatizo mengi katika baadhi ya jamii zetu. Baadhi ya mila na desturi haziwatambui watoto kama hao. Jamii zingine huwatupa watoto kama hao na kuwanyima urithi wa ardhi kwamba wataleta laana. Kwenye taasisi zetu kama vile shule, watoto wakati mwingine hupewa mafunzo yanayowahitaji wataje jina la baba yao. Inakuwa kero kwa watoto kama hao ambao hawajaonyeshwa baba yao au kuambiwa jambo lolote kuhusu aliyekuwa baba yao kwa wale ambao waliaga.

Katika uchunguzi wetu tulimpata mwanasanaa mcheza marimba na mwimbaji ajulikanaye Chizi maana yake ‘sura mbaya’ lakini mwenye maneno ya busara. Alieleza katika wimbo wake kuwa mama yake alikuwa ana sura nzuri lakini yeye ana sura mbaya na hamfahamu baba yake. Alipokuwa akimwuliza mama yake amwonyeshe baba yake, mama hakutaka mwambia. (UK.37.) Chizi aliwaambia wakaaji wa kijiji cha Patata wasihangaike na sura yake mbaya ila wayakabili matatizo ya Patata ambayo hakuelewa ayaite vita, ugonjwa au njaa. Baada ya kutafakari, alikata kauli kuwa matatizo ya Patata ni ‘njaa’ kama ile iliyokuwa ikimkabili kwa sababu ya uvivu ambao si kosa lake ila alifunzwa kuzurura. Njaa ambayo ilikuwa imeingia Patata ni ‘njaa ya kukosa umoja, ushirikiano, kuoneana wivu, na kuwa na uzembe mwingi. (UK.39.) Hizi ni baadhi ya sababu zilizosababisha NGUZO MAMA isisimame. Pia kwa sababu ya woga, wachache waliachwa kufanya walivyotaka. Hata ukweli walioujua, waliamua kunyamaza au kucheka huku vurugu zikizidi. (UK.40.) Baada ya vurugu kuzidi, mashauri yalifanywa na wakaamua kushirikiana. Ndipo ile NGUZO MAMA ikaanza kunyanyuka, lakini kabla haijasimama kabisa, wanachama walianza kutoweka mmoja baada ya mwingine kwa sababu ya tamaa. Kwa mfano BI MOJA alipomwona BI TANO akiwa na kanga mpya alitamani kujua zilikonunuliwa akamwuliza kuwa:

**BI MOJA**: *“Aisee hizo kanga mpya umenunua wapi?”*

**BI TANO**: *“Hee! Huna habari kuwa zimetoka? Hizi nimenunua jana pale kwa Mwarabu”.*

**BI MOJA***: Bado zipo?*

**BI TANO**: *Hata sasa hivi wanauza. Wewe tulipopita pale hukuona ile foleni?*

**BI MOJA***: anaachilia kamba na kuondoka.*

**BI NNE:** *Sasa jamani BI MOJA anakwenda wapi tena?*

**BI MOJA**: (*kwa mbali) Aaa jamani nitarudi. Lakini kanga hizi sizikosi.*

Baada ya BI MOJA kuondoka, mtoto wa BI PILI alifika na kumjulisha mama kuwa mtoto alikuwa akilia. BI PILI naye akaachilia kamba na kuondoka kwenda kumwona mtoto nyumbani. Ndipo walipokutana na mumewe akaanza kumhoji alikokuwa na kumwacha mtoto akilia. Jambo la kushangaza ni kwamba chakula cha mtoto kilikuwapo, lakini Sudi hangewezi kumpa kwa sababu hiyo haikuwa kazi yake kulingana na mila. Ni kazi ya mwanamke au mlezi. Hata kabla mama hajampa mtoto chakula na kumnyamazisha, Sudi alimwitisha nguo ya kuvaa na chakula ili aende kunywa pombe wenziwe wasimwache. Kwa bahati mbaya nguo ilikuwa imefuliwa lakini haikuwa imekauka. Mkewe alikuwa na majukumu mengi asubuhi ya lazima yaliyomzuia kumfulia mumewe nguo mapema. Kwa mfano kwenda shambani, kupikia watoto, na kuteka maji kutoka mtoni. Sudi hakuwa mtu wa kuelewa  wala hakutaka kujua ndiposa akamwambia mkewe kuwa aikaushe ile nguo kwa lazima akitumia moto ili atoke kwenda kunywa pombe. (UK.44.)

BI PILI aliyapitia maisha magumu mpaka ikambidi kutamani muujiza ufanyike ili apate mikono mingi tena mirefu ambayo ingemwezesha kufanya majukumu yote yaliyomkabili kama vile kulea mwana, kuwahudumia watoto na mumewe, kupika, kulima, kutenya kuni, kuchota maji na mwingine kuvutia Nguzo Mama.

BI TANO naye aliacha kuvuta kamba kwa sababu mumewe BI SITA alimkonyeza kwa ishara waende kuburudika. Kwa bahati mbaya BI SITA aligundua ujanja wao na kuanza kugombana. Kwa hivyo wote wawili wakaacha kuvuta kamba na makabiliano yakaanza moja kwa moja. Baada ya makabiliano, BI TANO alikaa chini na kuanza kuomboleza akisema:

**BI TANO:** *"Taabu! Taabu! Taabu!*

*Watoto wangu wanapata taabu*

*Hawana nguo hawana chakula*

*Watoto wanashinda njaa,*

*Wanalala na njaa*

*Mume wangu pesa zinaishia kwa wanawake*

*Nifanye nini mimi*

*Nifanye nini mimi taabu yote hii*

*Nifanye nini mimi taabu hii iniondokee!" (UK 49.)*

Msongo unaosababishwa na hali ngumu ya maisha umewafanya baadhi ya watoto na wazazi wao kuangamia kwa njia ya kusikitisha na kuhuzunisha mno. Kilio hiki cha BI TANO ndicho kilio cha baadhi ya wanawake waliotwikwa majukumu na malezi ya watoto peke yao. Ukabaila huu ulionekana kukithiri katika jamii ya mwandishi na pia ni kielelezo cha baadhi ya waume katika jamii zinazopatikana humu nchini. Mapato ya BI SITA yalitokana na biashara ya ukahaba uliomfanya kuwanasa wanaume wa kila tabaka jinsi mwandishi anavyotudokezea kuwa ilimbidi BI SITA kuwanasa wengi ili apate fedha za kumwezesha kukidhi gharama ghali ya maisha. Hali ambapo mwanamke anashiriki ngono na wanaume wengi haiwezi kumwepusha kupata watoto kutoka kwa wanaume tofautitofauti ikiwa mbinu za mpango wa uzazi hazitiliwi maanani. Hali hii ni yakini kwa baadhi ya wanawake ambao wamekosa kupata watoto kutoka kwa waume wa

ndoa na kutilia mashaka juu ya uwezekano wa kufanikisha kupata watoto kutoka kwao. Watajaribu kushiriki ngono na wanaume wengi ili kubahatisha kama wanaweza kupata mtoto.

Wanawake wengine hunyang'anywa watoto na kufukuzwa ili wanaowanyang'anya waweze kuhalalisha madai ya mali pengine ambayo imeachiwa mjane. Kiando na Makange walimvamia BI SABA na kumnyang'anya kila kitu nyumbani hata watoto kwa kuwa mumewe ambaye alikuwa ndugu ya Kiando na Makange alikuwa ameaga. Watoto ambao wameachwa yatima ni dhahiri kuwa baadhi yao hupitia maisha magumu kama vile BI MSIMULIZI anaeleza kuwa:

> **BI MSIMULIZI**: *"Bi Saba alitamani kufa mumewe kumfuata*
>
> *Alipoona wanawe wote watano*
>
> *Mdogo miaka mitatu*
>
> *Wanaswagwa kama mbuzi*
>
> *Eti waende kwa ndugu zao*
>
> *Huyo shangazi aliyewachukua*
>
> *Hata majina ya watoto wenyewe hayajui".(uk.53)*

Hizi ni baadhi ya sababu zinazowafanya wanawake kutoshiriki kikamilifu katika vikundi vyao vya harakati za kujikomboa kutokana na changamoto zinazowakabili. Changamoto hizi humfanya mtu kukosa raha na ile hamu ya kushirikiana na wanawake wengine. Wanawake wengine huona haya ya kujiunga pamoja iwapo wana dhani kwamba masaibu yao yanajulikana na kila mtu.

### 3.4 MAJUKUMU YA MWANAMKE NA NAFASI YAKE KATIKA JAMII

Majukumu ni sehemu ya maisha ya kibinadamu na ni wajibu wa kila mwanajamii kuwajibikia majukumu aliyopewa na kuyakubali kwa hiari. Lakini kwa bahati mbaya kuna baadhi ya wanajamii wanaotwikwa majukumu kupita kiasi kupitia taasisi za kijamii kama vile ndoa na tamaduni.

Mtunzi wa NGUZO MAMA anatupeleka hadi kijiji cha Patata ambapo kuna matata. Katika kijiji hiki tunawapata wanawake ambao wanajulikana kwa jina lingine kama wabeba wana wakijaribu kadri ya uwezo wao kuisimamisha NGUZO MAMA lakini wanashindwa kwa sababu ya majukumu mengi yanayowahitaji kutekeleza.Mtunzi aliamua kutumia Patata kama sehemu ambapo matukio yanafanyika lakini Patata inaweza kuwa kiwakilishi cha kijiji chochote humu duniani ambapo matukio yanayofanana haya tunayosimuliwa kwa njia ya mchezo wa kuigiza.

Wanawake wanahoji kuwa, ikiwa Nguzo Mama haitasimama, nyumba gani itasimama? Kwa njia nyingine wanawake wanahoji kuwa, ikiwa wanawake hawawezi kuungwa mkono kijamii, kiuchumi na kisiasa, ni jamii gani itakuwa na maendeleo? Wanaume wanawakabili kwa kuhoji:

**WANAUME:** "*Tangu lini wabeba wana kuwa watu?*" *(uk.57)*

Huu ni udhalilishwaji wa hali ya juu. Hili ni swali la mtu ambaye hana busara katika uteuzi wa maneno au mawazo. Katika hali yoyote ile, sote tukitathmini uwepo wa kila mmoja wetu humu duniani, ni kwa sababu ya hawa wabeba wana na wale wasio wabeba wana. Vile vile mtu yeyote anaweza kuhoji kuwa, ikiwa wabeba wana hawajakuwa watu, ni lini basi watakuwa watu? Swala la kimsingi hapa ni ubaguzi na utabaka kwa sababu ya majukumu mengi ya wanawake.

Hata hivyo kuna baadhi ya wanawake ambao hawatekelezi majukumu ambayo yanakubalika katika jamii. Kwa mfano BI SITA ambaye anajihusisha na ukahaba. Pia kuna wanawake amabao wana changamoto za kimaumbile ambapo si kosa lao.

Baadhi ya wanawake walio wazembe na ambao wana tamaa nyingi za kifantasia hawawezi kuridhika na maisha. Mara nyingi hawa hushinda ndani huku wamenyoosha miguu na kupiga domo. Wanawake wachache wenye bidii kazini kama BI PILI, hupatwa na tatizo la kuolewa na mabwana wanaofanana na Sudi mumewe BI PILI. Chizi anashangaa na kusema kuwa:

> **CHIZI:** *"Sijui mumewe kamlisha nini, kazi zote afanya BI PILI lakini mumewe ala matunda.Jasho la BI PILI linaishia kilabuni.Sudi anayatandika matindi usiku na mchana. (uk.60)*

Chizi alidhamiria kumwuliza Sudi amweleze dawa aliyokuwa amempa BI PILI ili naye ampe mkewe akubali kubeba mizigo yote-kuzaa watoto na kuwalea, kumlimia na kumpikia, kisha awe anamfulia nguo na kumpikia pombe

. BI NNE ambaye alibandikwa jina jipya-BI MANENO na Chizi, alieleza maazimio ambayo walikuwa wameyapitisha na mengine yalikuwa yameshaanza kufanya kazi. Baadhi ya maazimio haya yalikuwa malezi bora ya watoto, kufungua vituo vya watoto wadogo, kuanzisha miradi ya kila aina, vilabu vya pombe, maduka ya kuuza kanga, wanawake kupewa vyeo vya mawaziri, mameneja na mabalozi. (UK.64-65.) Haya yote ni baadhi ya majukumu.

Maazimio haya yalikuwa mazuri lakini yana changamoto za kipekee. Kwa mfano, BI SITA ni kahaba anayejisifu kuwa yeye ni breki tena ni jeki. Jeki ni kifaa kidogo sana lakini chenye uwezo wa kuinua kila aina ya gari. Majigambo haya ya BI SITA yanadhihirisha kuwa ana uwezo wa

kushiriki ngono na mwanaume yeyote bila kujali umri wala unene. Kuna wale ambao wamevurugiwa mawazo kama BI SABA.

Ushirikiano ni dhana muhimu sana kwa kundi lolote lile kwa ajili ya mafanikio ila si jambo rahisi kuafikiwa kwa sababu ya mitazamo tofautitofauti ya washirika.

Wakati mwingine inatubidi tujiulize, dunia hii ingekuwaje kama mwanamke hangekuwepo. Bila shaka taswira ambayo tungeweza kuwa nayo ni tofauti sana na ile tuliyo nayo kwa sasa. Mtazamo wa jamii hutegemea uchunguzi na uhakiki wa kazi za fasihi kama vile utenzi, nyimbo na michezo ya kuigiza ambayo ina mvuto wa kipekee kwa makundi mahususi na hatima yao katika jamii. Kulingana na nadharia ya sosholojia ya fasihi kuna mambo mengi yanayohusishwa na uchunguzi wa maumbo ya maandishi yanayoegemea hali ya kijamii.

Uchunguzi wetu ulionyesha kuwa mwandishi alidhamiria kubainisha umuhimu wa mwanamke katika jamii na changamoto zinazomkabili. Pia alinuia kuonyesha njia mbadala ambazo zinaweza kufuatwa ili kumpunguzia mwanamke changamoto hizo. Alijaribu kuangazia mbinu na mikakati wanayoitumia wahusika kujinusuru kutoka kwa mtanziko lakini bila kupata mafanikio ya kuridhisha. Baadhi ya sababu zinazoangaziwa kifasihi ni wivu, tamaa mbaya, chuki, hasira, kukosa umoja, na wanawake kuwa na malengo yanayotofautiana. Swala lingine nyeti ni utabaka ambao umekithiri miongoni mwa jamii zetu. Ndiposa Honore de Balzac (1799-1850) kama anavyonukuliwa na Coser (1963) akasema kuwa:

> *"ukiwa na familia ambazo uwezo unaolingana kimaisha katika sehemu yoyote ile utaona utabaka ukijitokeza hadharani, utawaona watu wangwana, wenye tabaka la juu na wenye tabaka la chini. Anaendelea kusema kuwa, 'usawa' ni haki, lakini hakuna mamlaka*

*duniani ambayo yanaweza kubadili kauli hii kuwa halisi"*. (Sociology Through Literature pp.133). ( tafsiri yetu)

Pili, alidhamiria kuonyesha kwamba mwanamke hawezi kufaulu kuupata uhuru na ukombozi wake wakati ambapo itikadi na mila potofu zina tawala au zina thaminiwa na jamii husika hadi pale mwanaume ataungana na kushirikiana naye. Tatu,mwanamke ni mshika dau katika mambo ya kijamii. Mwanamke na mwanaume wakikosa kushirikiana katika nyanja zote za maisha hatutakuwa na jamii iliyo na msingi thabiti. Mwisho, tabaka lolote haliwezi kuwa na nguvu au uwezo ikiwa halina njia za kuzalisha mali. Umiliki wa mali ni kipengele kinachochangia utabaka kuonekana wazi. Kuna njia za kuzalisha mali ambazo si nzuri kwa sababu zina athari hasi. Kwa mfano ukahaba, kuuza pombe haramu ambayo haijakaguliwa na wakaguzi wa ubora wa bidhaa, na kuuza aina mbalimbali za mihadarati.

## 3.5 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA NGUZO MAMA

Mwandishi anapoandika huwa na maksudi ya kipekee ambayo yanaweza kuwa zaidi ya kile msomaji anatafuta au anafikiria. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi inaruhusu mitazamo tofauti baina ya mwandishi na msomaji.

Ndio maana katika kazi ya uchambuzi, mhakiki anaweza kuzua maswala anuwai. Kulingana na uchambuzi wetu, msanii alimchora mwanamke kama kiumbe dhaifu. Udhaifu huu ni wa kiuchukulizi, si hali asilia ambayo mwanamke huzaliwa nayo. Ndiyo maana ya ile NGUZO MAMA kubakia pale chini licha ya juhudi nyingi zilizofanywa kuisimamisha. Hii ndiyo pia sababu iliyomfanya BI NANE kutoa wazo la kuwahusisha wazee na watoto kwenye harakati za kuisimamisha *Nguzo Mama*. BI MOJA anasema:

**BI MOJA**: *"Uvivu unaturudisha nyuma sisi." (UK. 22.)*

Pili mwanamke alichorwa kama mtu ambaye hana ruhusa ya kumiliki mali ya mumewe endapo mume ataaga. Ili kudhihirisha kauli hii, BI SABA alinyang'anywa kila kitu hata ufagio baada ya mumewe kuaga. Kuna baadhi ya jamii ambazo zinashikilia msimamo huu. Hata hivyo, jamii nyingi hazitilii maanani dhana hiyo.

Tatu, mwanamke anachukuliwa kuwa mdanganyifu na mwenye maringo. Taswira hii ilionyeshwa wakati BI TANO na BI SITA waligombana na kutukanana. (UK.47-48.) Baadhi ya wanawake walichorwa kama kupe (wanyonyaji) ambao hawakutaka kufanya kazi lakini wakaonekana wenye mahitaji ya juu kwa mfano, BI SITA aliyesema:

> **BI SITA**: *"waachie wale wajinga, muda waupoteza. Mwenzao nautafuta huo muda siupati. Laiti ningepata wengi zaidi kunasa. Kwani mmoja wawili wanafaa kitu gani. Bei zenyewe hizo za kuruka."* (uk. 50).

Mwanamke alichorwa kama mtu mwenye tamaa. Kwa mfano, BI MOJA alipomwona BI TANO amejifunga kanga mpya ambayo alikuwa hajawahi kuona alikuwa na shauku ya kujua ilikopatikana. Baada ya kufahamu sehemu aina ya kanga zile zilikuwa zikiuzwa aliacha shughuli ya chama na hata akajaribu kupigana na Shabani na kumlazimisha ampe hela akanunue kanga na akaapa kuwa hawezi kuikosa. (UK. 42-43.)

Mwanamke amechorwa kama mtu mwenye chuki na wivu. Kwa mfano BI NNE alipomshambulia BI NANE, na kusema:

> **BI NNE:** *"Hayo madigrii wanayoringia anataka kuyaleta hapa."* (UK.32.)

Kulingana na Indede Florence (2011), Ushairi wa 'Karne Mpya' umejitokeza na taswira ya kuogofya ya mwanamke. Wanamashairi wanayawasilisha matendo halisi na matukio katika jamii

zao na hatuwezi kuwalaumu kwa wanayowasilisha. Umbo tunalolipata katika ushairi wa karne hii kwa kweli si umbo la mwanamke kuwa ua au pambo bali chombo cha madhila na unyanyasaji katika matukio ya aina tofauti kutokana na maisha ya kindoa, siasa, dini, vita na kazi. Anapendekeza kuwa, ili kujikomboa na kujinasua kutokana na minyororo ya ukandamizwaji wa kijamii wasanii (wanafasihi) wajitokeze kama watetezi wa haki na ukombozi wa mwanamke katika ngazi mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa, na kijinsia. Kwa mfano, Mohamed S. (2010), alichukuwa hatua katika shairi lake *'kama wanipenda kweli'* na kuandika kuwa:

*"kama wanipenda kweli sinifanye wako nyuni*

*Sinifungie tuduni niache niruke huru*

*Au sinifanye asumini sinishabihi zabibu*

*Niite mtu kwa dhati."*

Pia Mohamed S.A.(2002) ameaandika katika shairi *'mwanamwari wa kesho'* kuhusu heshima ya ubinadamu usawa na uhuru kuwa:

> *"Mwanamke si mtumwa tena, si mtawa tena ingawa yu ndani mwake, si mteteti tena ingawa umbile lake, si hawara tena ingawa hiari yake, si Malaya tena hata hivyo watamke. Atakuwa huru usoni mwa babake."*

Ndiposa Mohamed anashauri kuwa:

*"Maisha ni ubishi, bishana nayo.*

*Maisha ni vita, vikabili!*

*Maisha ujasiri, jusurisha!*

*Maisha ni huzuni, ziepuke!*

*Maisha ni wajibu, tekeleza.”*

Mitazamo mbalimbali kuhusu taswira ya mwanamke ni mada ambayo waandishi wengi watazidi kuangazia na kutoa mwongozo mwafaka kwa jamii zote ili kumchukua mwanamke kwa mtazamo chanya utakaohakikisha kuwa amepewa hadhi na haki za kibinadamu.

# SURA YA NNE

# WAHUSIKA NA MANDHARI KATIKA TAMTHILIA ZA *NGUZO MAMA* NA *MAMA EE*

## 4.0 UTANGULIZI

Wahusika ni kipengele cha fani tulichotaja hapo awali kuwa tutaangazia katika kazi hii. Vipengele vya fani ni vingi lakini kulingana na mpangilio wa kazi hii tuliamua kushughulikia wahusika, mandhari na maudhui. Hii ni kwa sababu wahusika hutumiwa ili kutekeleza uamilifu au jukumu la kimaudhui. Wahusika wetu tumewaangazia kwa mkabala wa kimwingiliomatini ambapo tumejikita kwenye wasifu na migogoro waliyokumbana nayo.Baadhi ya migogoro tuliyotambua ni ugomvi wa kifamilia unaochangiwa na ulevi, ubaguzi na uonevu wa mwanamke, ukandamizwaji wa mwanamke, ukabaila na umwinyi wa wanaume na ukosefu wa umoja na ushirikiano baina ya wanawake miongoni mwa mingine. Hatuna budi kulinganisha na kulinganua jinsi waandishi wa matini zote wametubainishia taswira ya mwanamke kupitia matendo na mazungumzo ya wahusika.

## 4.1 DHANA YA WAHUSIKA

Wahusika ni wale watu au vitu vinavyosababisha matukio fulani kutokea au kutendeka.

Msokile M. (1993) ametubainishia wahusika kama vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa. Pia mimea, mashetani na mizimwi yanaweza kuchukua nafasi ya wahusika.

Wamitila K. (2008) ametubainishia wahusika kuwa watendaji wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi za kifasihi. Ni vielelezo vinavyowakilisha viumbe wanaopatikana ulimwenguni. Kiini cha uchunguzi wa wahusika katika

kazi yoyote ya fasihi ni kutaka kuelewa tabia na mienendo yao, wasifu wao, hisia na fikra zao, mahusiano yao, mazingira yao na falsafa zao.

Baadhi ya kazi za kifasihi zina wahusika ambao huzua migogoro na wengine hujaribu kutatua migogoro hiyo. Mwandishi wa kazi ya fasihi huwasawiri wahusika wake kulingana na malengo yake. Kuna wale wanaoamini kuwa kazi ya fasihi haitakuwa imekamilika bila mgogoro au migogoro. Sisi hatukubaliani na kauli hii ila tunakubaliana kuwa kazi za kifasihi ambazo husisimua hadhira ni zile zenye migogoro au vichekesho.

Sifa na wasifu wa mhusika hubainika kutokana na matendo yake au maelezo yanayotolewa na mwandishi mwenyewe au mhusika mwingine.

## 4.2 MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA *MAMA EE* NA *NGUZO MAMA*

Maudhui ni mafundisho yenye umuhimu fulani yanayowasilishwa kwa hadhira kupitia kazi za kifasihi. Mwandishi hutumia 'nyenzo' au 'fani' ili kufikia lengo hili. Maswala yanayoshughulikiwa katika tamthilia za *Mama Ee* na *Nguzo Mama* yamejitokeza kupitia wahusika na matendo yao.

Maudhui makuu ambayo waandishi waliyaangazia ni ya kijamii hasa kuhusu maswala ya taswira ya mwanamke, unyumba, uchumi, mila, utamaduni na mitazamo tofautitofauti.

Mazrui na Syambo (1992) wanadai kuwa:

> "Mtunzi wa riwaya, kwa mfano, ana njia nyingi za kueleza lolote analotaka kutueleza. Lakini mwandishi wa tamthilia ana njia moja tu, nayo ni mazungumzo ya wahusika wake…..Ingawa hadithi ya tamthilia ni mfululizo wa matukio kama

hadithi yoyote nyingine, mwandishi hulazimika kuvunjavunja mfululizo huo katika sehemu za matendo na maonyesho, ili aweze kuichukua hadhira mbele na nyuma, na hapa na pale."

Taswira ya mwanamke imeangaziwa na waandishi wote wawili wamemsawiri mwanamke kwa njia ya kipekee kwa kuwatumia baadhi ya wahusika wao.

Ifuatayo ni baadhi ya taswira ya mwanamke kupitia wahusika: Mwanamke ni mdhaifu akilinganishwa na mwanaume. Wahusika wote BI MOJA hadi BI NANE walijaribu kuinua Nguzo Mama wakashindwa. Huu ni uchukulizi wa kawaida. BI MOJA anatuthibitishia kauli hii anaposema:

**BI MOJA**: *"Nakwambieni uvivu utaturudisha nyuma sisi". (uk.22)*

Mwanamke amechorwa kama mtu mwenye tamaa. BI MOJA ni mhusika aliyetumiwa na Muhando kwa kuwa alipomwona BI TANO akiwa na kanga mpya alidhamiria kujua zilikonunuliwa ajinunulie aghalabu jozi moja. BI SITA pia alitumiwa kwa sababu alitamani kuwanasa wanaume wengi.

Mhusika BI NNE alimshambulia BI NANE na kumweleza mwenyekiti wa wanawake kuwa:

**BI NNE:** *" Hayo madigrii wanayoringia anataka kuyaleta hapa". (uk.32)*

Usemi huu unaonyesha kwamba mwanamke ana taswira ya chuki na wivu kwa mwanamke mwenzake.

Mwanamke amechorwa kama mwoga. Tenge na mamaye wanamshauri Mwavita arudi kwa Kinaya kwa sababu asiporudi atazaa nje ya ndoa aitwe hawara na kila mtu. Mamake Tenge

anamdadisi Tenge ili afahamu kama Tenge amepata mimba ya pili. Haya yote ni kwa sababu ya woga wa mwanamke. Maudhui mengine yanayoshughulikiwa na waandishi katika tamthilia hizi ni ya uchumi na nyenzo za kiuchumi.

Uchumi ni miongoni mwa mambo muhimu ya kimsingi kuhusu maisha ya kibinadamu. Ni kiunzi muhimu ambacho pia ni chanzo cha matatizo mengi na migogoro ya kisiasa na kiunyumba. Ni bayana kwamba mtu ambaye hajiwezi kiuchumi hukumbwa na matatizo mengi kama vile kubaguliwa, kudhulumiwa, kudharauliwa na hata kunyimwa nafasi ya kuwa kiongozi.

Maudhui ya unyumba yameshughulikiwa na waandishi hawa Muhando na Mwachofi. Mwachofi ameliangazia swala hili kwa kuwatumia wahusika wakuu Kinaya na Mwavita. Matatizo ya unyumba yanapokuwa sugu yanazua taharuki na kuleta athari mbaya kama vile kutengana, msongo, kuwanyima watoto malezi bora yaliyo na amani na kuleta aibu kijijini kupitia ugomvi na marumbano ya kila mara. Naye Muhando ameangazia swala la unyumba kwa kuwatumia wahusika Sudi na BI PILI mkewe. Sudi ni mlevi sugu kama Kinaya. Wote wawili wana tabia ya kuwahangaisha wake zao kwa sababu ya ulevi wa kupiga matindi kupita kiasi, jambo ambalo limewafanya kutumia rasilimali na muda, na kuipuuza familia. Pia Muhando amemtumia BI MSIMULIZI kutusimulia jinsi BI SABA anavyohangaishwa na shemeji zake Kiando na Makange baada ya mumewe aliyekuwa mlevi sugu kufariki. BI MSIMULIZI anaeleza:

> **BI MSIMULIZI***: "Akalia BI SABA tena akalia*
>
> *Hana wa kumsaidia*
>
> *Mumewe kafa nduguze wamekuja juu*
>
> *Pesa wamechukua senti tano haikubaki*

*Vyombo na nguo zote wakagawana*

*Roho ilimpasuka Bi Saba kuwaona hao ndugu*

*Walivyoigombania mali wasiyo ichuma*

*Hata ufagio wamebeba*

*Watoto wake wapenzi mwenyewe aliwalea*

*Wakati wao baba matindi akiyachapa*

*Na pesa kwa pombe kuangamiza*

*Pesa ya ndugu yao iliishia chooni".*

Majukumu na uwajibikaji ni maudhui ambayo yameangaziwa kwa mapana na waandishi hawa. Majukumu kama vile ya wazazi, mahakama, watoto, wanafunzi, wanawake, wanaume, na dini miongoni mwa mengi yameguziwa japo si na waandishi wote. Tuligundua kuwa kuna baadhi ya wahusika walioyachukua majukumu yao kiholelaholela na kuna wengine waliotilia maanani majukumu yao na kuwajibika kisawasawa. Kinaya, Padre, Tenge na George ni mifano ya wahusika katika tamthilia ya *Mama Ee* walioyachukua majukumu yao kiholelaholela. BI TATU, Sudi, Makange, Kiando na mumewe BI SABA ni wahusika katika tamthilia ya *Nguzo Mama* ambao hawakuyawajibikia majukumu yao sawasawa.

Ukosefu wa maadili ni swala ambalo linaonekana kuongezeka siku za hivi karibuni. Waandishi wote wawili waliwatumia wahusika wachache kuangazia swala la kimaadili japo si kwa undani sana. Mwachofi aliwatumia Tenge, George, na Kinaya kuonyesha jinsi maadili hayatiliwi maanani na baadhi ya wanajamii jambo ambalo limeleta uozo katika jamii. Naye Muhando alimtumia mhusika BI SITA kuangazia swala hili.

Wamitila (2008) kama alivyomnukuu Aristotle katika andiko la *Poetics,* anasema:

> *"Aristotle alishikilia kuwa wahusika wa tanzia huwa na hadhi kubwa kijamii ili kuhalalisha anguko lao baadaye ambalo hutokana na udhaifu wao kama binadamu. Wahusika wanaofungamanishwa na visasili, husawiriwa wakiwa na sifa fulani ambazo zinawakweza juu ya watu wa kawaida-na kwa njia hii wahusika wengine wanaoweza kupatikana katika tamthilia nyingine zinazohusishwa na visasili……………"*

Majukumu ya wahusika katika kazi ya fasihi yoyote ile ni muhimu kwa sababu dhamira za waandishi haziwezi kubainishwa bila kuwatumia wahusika. Mara kwa mara wahusika hubainishwa kupitia usemi wa lugha wanayotumia au maelezo yanayotolewa na wahusika wengine. Pia matendo ya wahusika hutudokezea wasifu wa kila muhusika. Kwa mfano; katika tamthilia ya Nguzo Mama BI SITA anasema:

**BI SITA:** *"Mji huu sikuingia leo ndugu yangu*
*Mawaziri makabwela mapadre kwa*
*Mashehe vijana kwa wazee*
*Mie breki mie jeki*
*Kwangu mie utasimama."*

Swala ambalo BI SITA analizungumzia kupitia usemi wake linatudokezea kuwa yeye ni mtu ambaye ameamua kwenda kinyume na maadili ya jamii. Yeye hachagui mtu wa kwenda naye kwenye starehe zake. Anaashiria jinsi jamii imekuwa na uozo kimaadili. Ni kupitia kwa usemi wake mwenyewe tunamwelewa BI SITA kuwa ni mwanamke wa aina gani kitabia.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 UTANGULIZI

Tulidhamiria kuchambua na kuhakiki tamthilia mbili *Nguzo Mama* na *Mama Ee* kwa kuangazia 'taswira ya mwanamke'. Ili kuafiki malengo yetu ilitubidi kudurusu na kusoma matini mbalimbali ambazo zilituwezesha kufika hatua hii. Shughuli hii haikuwa rahisi lakini kwa sababu ya wasimamizi wenye tajriba ya kutosha na uzoefu wao, shughuli ya uchunguzi na uandishi wa kazi hii umetekelezwa kwa ushirikiano wa dhati.

Ni muhimu kutaja hapa kuwa shughuli ya kufanya uchunguzi wa swala lolote lile utafanikiwa tu, ikiwa mchunguzi atashirikiana na kufuata maagizo ya wasimamizi jinsi wanavyomwelekeza. Mchunguzi anatakiwa kuwa huru na wasimamizi na kuwauliza pale ambapo anakumbana na shida au ugumu fulani. Vile,vile ni jambo la busara kushirikiana na watafiti wengine ili kubadilishana mawazo ambayo yatachangia kuikamilisha kazi ya mtu binafsi.

### 5.1 MUHUTASARI

Msukumo wa kazi hii ulitokana na tatizo la utafiti kuhusu migogoro inayopatikana katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee*. Ilibainika kuwa changamoto zinazomkumba mwanamke katika jamii za waandishi wa tamthilia hizi, zinafanana licha ya kuandikwa vipindi tofauti na waandishi tofauti.

Sisi tulitumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kama dira iliyotuongoza katika utafiti wetu. Kuna nadharia kadhaa ambazo hutumiwa katika uchunguzi wa maswala yanayohusiana na jamii. Nadharia hizi ni U-Marx, Uhalisia wa Kijamaa, Uhalisia, Umuundo na Sosholojia ya Fasihi. Tulichagua kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kwa sababu haijatumiwa sana katika uchunguzi unaohusiana na maswala ya kijamii.

Tuliweza kubainisha jinsi changamoto zinazomkabili mwanamke zimechangia kutofaulu kupata haki. Kwa mfano, ubaguzi, unyanyaswaji, utabaka, majukumu mengi, kukosa umoja miongoni mwa nyingine. Majukumu mengi ya mwanamke yalionekana kuwa huchangiwa na asasi za kijamii kama vile taasisi za ndoa, utamaduni, mila na desturi.

Ilibainika kuwa Muhando na Mwachofi wamewasawiri wahusika hawa Mwavita na BI NANE kama nguli. Hata kama pale mwishoni walionekana kushindwa, ujasiri wao ulidhihirika kulingana na hatua mbalimbali walizochukua ili kukabiliana na changamoto za mwanamke na kupigania haki za mwanamke.

Tulichagua mada ya 'taswira ya mwanamke' kwa kuangazia tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee kwa sababu ya fani na maudhui yanayofanana na jinsi hali halisi ilivyo katika jamii zetu.

**5.2 HITIMISHO**

Katika utafiti wetu tuliweza kugundua kuwa mwanamke anakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zimemfanya akose uhuru kamili wa kujiamulia baadhi ya maswala ya kijamii na kiuchumi. Changamoto hizo zinafungamana na taasisi za kijamii kama vile tamaduni, ndoa, dini,

elimu na miiko. Pia tuligundua kuwa changamoto hizo zinamfanya mwanamke kuwa na taswira mbalimbali ambazo zinamdhalilisha licha ya kuwa nguzo muhimu katika ukuaji na maendeleo ya jamii.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Ili utafiti wowote uweze kuwa wa manufaa kwa jamii ni lazima mtafiti aweze kutambua mwanya ambao utahitaji kuzibwa na watafiti wa baadaye. Kwa muktadha huu tunatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye.

i) Swala la dini kuchangia katika unyanyaswaji wa mwanamke yafaa lichunguzwe kwa jicho pevu.

ii) Changamoto zinazomkumba mwanamke katika jamii zetu zitafutiwe suluhu la kudumu.

iii) Kuna pendekezo kutoka kwa baadhi ya wanaharakati wa mrengo wa kifeministi kuwa wanawake wasusie taasisi ya ndoa. Swala hili lichukuliwe kuwa nyeti.

## MAREJELEO.


Beauvoir, S. (1949): *The Second Sex.* Pan Books Publishers, London.

Coser,L(1963): *Sosiology through literature: an introductory reader.* Prentice Hall. Englewood Cliffs.

Indede, F. (2011): *Mwanamke angali tata katika ushairi wa kisasa?* www qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documens

Iribemwangi na Mukhwana. (2011): *Isimujamii.* Focus Publishers Ltd. Nairosbi .

wa Mberia,K. (2007): *Natala.* Marinba Publication L

td. Nairobi, Kenya.

Madumulla, J S. (2009): *Riwaya ya Kiswahili:Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi.* Nairobi. Sitima Printers &Stationers Ltd.

Mbuthia, E. M. (2005): *Astylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories.* A PhD thesis of the University of Nairobi.

Mirikau, S. A. (2011): *"Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila K. W*." Tasnifu ya Shahada ya uzamili chuo kikuu cha Nairobi.

Mohamed, S. A. (2010): *Nyuso za wanawake*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Msokile, M. (1993): *Misingi ya uhakiki wa fasihi.* East African Educational Publishers Ltd. Brick court, Mpaka Rd/Woodvale. Nairobi.

Muhando, P. (2010): *Nguzo Mama.* Muwa Publication Ltd. Nairobi, Kenya.

Mukobwa, M (1985): *"Maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia tano za Ebrahim N. Hussein".* Tasnifu ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi.

Murori, K.(2012): *The Winning Character*. Nairobi. Queenex Publishers Limited.

Mwachofi, A. K. (1987): *Mama ee.* East African Educational Publishers. Nairobi.

Mwita, B. M.(2005): *"Dhima ya ichingero za Wakuria katika kusawiri taswira ya mwanamke".*
Tasnifu ya shahada ya uzamifu ya chuo kikuu cha Moi.

Narizvi, S. (1982): *The sociology of the literature of politics*. Australia. Edmund Burke

Ngugi, G.(2011):*Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi*. East African Educational Publishers Ltd.
Nairobi.

Nguta, (2011): "*Fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya Pango na Mama ee*."
Tasnifu ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi.

Njagi, F. (2011*). "Peaceful Families."* (family life week study guide). Nairobi: East African
Union Division of S.D.A.

Ntarangwi, M. (2004): *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Islands.Augustine college.

TUKI (2002): *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Published by O.U.P. East African Ltd.ABC place
Nairobi.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007): *Nadharia Za Uhakiki Wa Fasihi*.Jomo Kenyatta
Foundation. Nairobi, Kenya.

Wamitila, K. (2012): *Nguvu Ya Sala.* Longhorn Publishers. Nairobi, Kenya.

__________ (2003): Pango. Focus Publication Ltd. Nairobi, Kenya.

__________ (2008): Misingi ya uchanganuzi wa fasihi.Nairobi. Sitima Printers & Stationers Ltd.

Wellek & Warren. (1954). *Theory Of Literature*. London.